# Nipashe

Jumamosi Septemba 21, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581806

www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US




RUBY USISEME YOTE

UKURASA 12

UKURASA WA 2

**Dk.** Biteko atoa maagizo matano ufuatiliaji, tathmini



UKURASA WA 3 & 4

**ACT** Wazalendo yanusa harufu rushwa Ardhi, waziri alonga

UKURASA WA 15

**Wabaini** tatizo katika nyimbo na mavazi ya wasanii nchini




## TIBA YA KIBINGWA

# Aondolewa uvimbe kilo 5 Muhimbili

- **Ni** aliyeibuliwa na wanahabari; bingwa afafanua undani wa ugonjwa huo hatua kwa hatua... *Endelea Ukurasa 2*

# Polisi yazuia mkutano wa Tundu Lissu

UK. 18



Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza na Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, IGP Camillus Wambura pamoja na Makamishna wa Jeshi hilo Ikulu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# Atiwa mbaroni kwa tuhuma kumtoboa macho mtalaka

UK. 8

**MICHEZO** **MPANZU AWASILI NCHINI KUMALIZANA NA SIMBA** UK.24

**MAONI,** UK.6

# Naibu Waziri Mkuu atoa maagizo matano ufuatiliaji na tathmini

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko amezitaka taasisi za ufutiliaji na tathmini kufanya kazi kwa weledi na kuimarisha eneo hilo ili kuendana na mahitaji yanayolenga kuleta tija katika utoaji huduma kwa wananchi.

Alielekeza hayo jana Zanzibar wakati akimwakilisha Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa katika Kongamano la Tatu la Ufuatiliaji, Tathmini na Kujifunza.

Dk. Biteko alisema wataalamu wa ufuatiliaji na tathmini wanawajibika kulinda taaluma hiyo na kuwashawishi kwa hoja wakuu wa taasisi husika kupenda kazi zinazotokana na taaluma hiyo badala ya kujisikia wanyonge kitaaluma.

Naibu Waziri Mkuu Biteko aliwataka washiriki muda wote kusisitiza misingi ya taaluma hiyo na baadaye kuleta matokeo chanya kwa maendeleo ya taifa na watu wake.

"Inawezekana katika maeneo yenu ya kazi wakawapo wakuu wa taasisi au viongozi wa serikali ambao hawapendi mfanye kazi yenu vizuri, kukubaliana na hilo ni kujiua wenyewe.

"Mnapotoka hapa mkafanye mkuu wa taasisi au kiongozi aone umuhimu wenu katika shirika," aliagiza Naibu Waziri Mkuu Biteko.

Aliwataka wataalamu hao kusema ukweli na kusimamia taaluma yao, akisema "Ninataka niwaombe mkajiamini, Rais Samia ameagiza na kuelekeza kuwapo vitengo vya tathmini ndani ya serikali.

"Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji wafanye kazi na kitengo cha ufuatiliaji kilichopo Ofisi ya Waziri Mkuu, mfuatilie fedha zinazopelekwa kwenye miradi na matokeo yake kwenye kubadilisha hali za maisha ya watu," alisisitiza Dk. Biteko.

Kupitia kikao hicho, Naibu Waziri Mkuu alitoa maagizo matano yakilenga kuboresha ufuatiliaji, tathmini na kujifunza.

"Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu ikamilishe mapema Mfumo Ufuatiliaji na Tathmini na kuwezesha taarifa za utendaji wa Serikali kupatikana kwa urahisi.

"Tume zetu za Mipango zikamilishe uchambuzi wa miradi yote inayotekelezwa ndani ya serikali na kila mwaka kutoa taarifa ya utekelezaji. Namna hii itawezesha serikali kuona tija ya miradi inayoidhinishwa na kutekelezwa nchini," aliagiza.

Dk. Biteko alielekeza ofisi hiyo kukamilisha Sera ya Kitaifa ya Ufuatiliaji na Tathmini ili iweze kuleta utekelezaji sahihi wa eneo la ufuatiliaji na tathmini nchini.

Aliagiza TanEA na ZaMEA kuwa sera pamoja na mikakati yake viwe zinafanyiwa tathimini kila baada ya miaka mitatu baada ya kuandaliwa.

"Hii itasaidia kujua kila hatua inayofikiwa kwa utelezaji wake pamoja na utatuzi wa changamoto za utelezaji na maboresho wakati wa uhuishaji sera," aliagiza.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu, William Lukuvi alisema Kongamano hilo la tatu la Ufuatiliaji, Tathmini na Kujifunza limepata mwitikio mkubwa kutoka kwa wadau na washiriki.

Alitaja lengo la kongamano hilo kuwa ni kuweka msisitizo kwenye lengo kuu la serikali la kutoa huduma bora na kwa wakati kwa wananchi na kuwa katika kutimiza azma hiyo, washiriki wakihamasishwa kutumia vizuri taaluma na mafunzo mbalimbali wanayoyapata kuhakikisha wanakuwa jicho la serikali katika mipango yake, utendaji wake na utekelezaji miradi.

Lukuvi alisema Rais Samia Suluhu Hassan pamoja na Rais Hussein Ali Mwinyi wamekuwa vinara wa ufuatiliaji na tathmini katika utendaji wa serikali kwa ujumla wake, utekelezaji wa miradi yote nchini na utoaji huduma bora kwa wakati kwa wananchi wote.

Alisema kuwa marais hao wanafanya hayo ikiwa ni utekelezaji Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020 ambapo kwa sekta zote umewekwa mkazo wa ufuatiliaji na tathmini katika utendaji, utekelezaji miradi na utoaji huduma.

"Katika kuimarisha Sekta ya Fedha, ibara ya 20(f) ya Ilani ya CCM inaitaka serikali kuimarisha ufuatiliaji na tathmini ya mashirika na taasisi zilizobinafsishwa ili kuhakikisha mikataba inatekelezwa ipasavyo na sekta ya ujenzi, ibara ya 51(a)(ii) ya Ilani inaitaka serikali kuboresha mfumo wa ufuatiliaji na tathmini wa shughuli za barabara kwa kuhakikisha thamani ya ubora wa kazi inaendana na fedha zilizotumika," alisema Lukuvi.

Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Dk. Jim Yonazi alisema kuwa kupitia kongamano hilo wamepata fursa mbalimbali ikiwamo kuwa na mchango mkubwa katika kuongeza uwezo wa wataalamu.

Kaimu Katibu Mtendaji Tume ya Mipango, Dk. Ameir Haji Sheha alisema kongamano hilo limejumuisha washiriki 738, akishukuru Ofisi ya Waziri, Sera, Bunge na Uratibu kwa ushirikiano wakati wote wa maandalizi wa kongamano hilo.



Naibu Kamishna wa Polisi (DCP), Mwamini Rwantale na Mkuu wa Chuo cha Taaluma ya Polisi Kurasini, DCP Dk. Lazaro Mambosasa, wakikata utepe kuzindua maadhimisho ya Siku ya Uchunguzi wa Kisayansi Duniani, chuoni hapo, Dar es Salaam jana.
**PICHA: JUMANNE JUMA**

MATIBABU YA KIBINGWA

# Arejeshewa tabasamu baada ya kuondolewa uvimbe wa kilo tano

**Na Romana Mallya**

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili (MNH) imemrejeshea tabasamu Karume Karume (41) baada ya kufanyiwa upasuaji rekebishi kwa kumwondoa uvimbe wa kilo tano uliomsumbua kwa zaidi ya miaka 25.

Karume ambaye ni mkazi wa Lindi, alikuwa anasumbuliwa na uvimbe sehemu mbalimbali za mwili wake, Baada ya upasuaji huo, ameruhusiwa kwenda nyumbani.

Bingwa Mbobezi wa Upasuaji Rekebishi na Mkuu wa Kitengo cha Upasuaji Rekebishi, Dk. Laurean Rwanyuma, aliongoza jopo la wataalamu wenzake kumfanyia upasuaji uliodumu kwa saa nne.

Alitoa ufafanuzi huo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu upasuaji huo, akisema kuwa baada ya uchunguzi wa kina kukamilika, iligundulika kuwa Karume alikuwa na uvimbe sehemu mbalimbali za mwili wake hasa shingoni, begani na kifuani na ugonjwa huo kitaalam unaitwa 'Plexiform Neurofibromatosis'.

Alisema matibabu ya ugonjwa huo ni kuondolewa kwa njia ya upasuaji. Agosti 30 mwaka huu walimfanyia.

Dk. Rwanyuma alisema ugonjwa aliopata Karume si wa kuambukiza, bali ni wa kuzaliwa nao, akiurithi kutoka kwa wazazi wake au mzazi mmoja.

Alisema ugonjwa huo hushambulia mishipa ya fahamu na kujitokeza kwa njia mbalimbali.

Dk. Rwanyuma alisema mtu anapata ugonjwa huo kutokana na kurithi vinasaba kutoka kwa wazazi na si kila mtoto anaweza kuwa navyo.

Alisema matibabu yake kama uvimbe utakuwa mkubwa, ni kukata na upo uwezekano wa uvimbe huo kurejea tena.

"Unaweza kurejea baada muda kama miaka mitano. Mtu anaweza kupata uvimbe ambao ni mkubwa sana, unakuwa mzigo kwake.

"Wapo wanaopata usoni, unaondoa mwonekano, hivyo unaondolewa ili kumwezesha kufanya shughuli zake za kila siku. Wagonjwa wa namna hii ambao tunawapokea hospitalini hapa kwa mwezi huwa hadi watano," alisema.

Mtaalamu huyo pia alisema wapo wanaorithi vinasaba vya ugonjwa huo, lakini uvimbe ukawa mdogo.

"Kama umemwona mama yake Karume, yeye anavyo vidogovidogo ambavyo havihitaji upasuaji.

"Wito wetu; mtoto anapozaliwa basi aangaliwe kama ana alama yoyote. Dalili za ugonjwa huu unakuta mtoto ana baka mwilini.

"Huwa na rangi kama chai ya maziwa iliyowekwa kahawa, ukiona hivyo, fika kwa wataalamu ili kubaini kama ni ugonjwa huu," alielekeza.

Mkurugenzi wa Huduma za Upasuaji, Dk. Rachel Mhaville, akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali hiyo, alisema mara baada ya kumpokea mgonjwa huyo mwezi uliopita, hospitali ilifanya jitihada za dhati kuhakikisha anaonwa na madaktari bingwa na kufanyiwa vipimo mbalimbali.

"Tunawapongeza waandishi wa habari kwa kumwibua mgonjwa huyu na kumleta hospitalini, kwani ndipo penye madaktari bingwa bobezi wa upasuaji rekebishi walioweza kumpa huduma stahiki na kumrejeshea mwonekano unaompa faraja na tabasamu," alisema Dk. Mhaville.

Aliwaomba wasamaria wema kuendelea kujitokeza kuchangia huduma kwa watu wasiokuwa na uwezo, akiwamo Karume ili kukamilisha malipo ya huduma alizopata kupitia namba ya malipo 994501766575 yenye jina Hospitali ya Taifa Muhimbili.

Mjomba wa Karume, Salum Idobelele, alisema alihangaika na Karume tangu akiwa na umri wa miaka 16 baada ya kupata uvimbe huo.

"Mwaka huu ndipo alipokutana na waandishi wa habari kupitia Chama cha Waandishi wa Habari Mkoa wa Dar es Salaam ambao walibeba jukumu la kumtafutia msaada wa matibabu kwa kumpeleka Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Temeke na kisha kupewa rufani kwenda Muhimbili.



Mkurugenzi wa Kituo cha Ubia (PPP), David Kafulila (kulia), akipokea zawadi kutoka kwa Mkuu wa Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), Prof. Edda Lwoga, wakati wa mkutano na wadau mbalimbali, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu ujenzi wa mabweni ya chuo hicho kwa ubia. **Habari Uk. 7. PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# ACT yadai kunusa harufu ya rushwa mabaraza ya ardhi

**Na Halfani Chusi,** KITETO

KIONGOZI wa Chama cha ACT Wazalendo, Dorothy Semu, amekemea kile alichokiita "rushwa kwa baadhi ya viongozi katika mabaraza ya ardhi", akidai hali hiyo inachangia kuwapo migogoro ya kudumu.

Dorothy alitoa kauli hiyo juzi wilayani Kiteto, mkoani Manyara, akiwa katika mwendelezo wa ziara zinazofanywa na viongozi wakuu wa chama hicho waliojigawa kikanda.

Alisema Kiteto ni "ni moja ya makao makuu ya migogoro ya ardhi" ambayo inasababishwa na mgongano kati ya wakulima na wafugaji.

Alisema changamoto hiyo si ya Kiteto peke yake, bali iko katika maeneo mengi, ikihusisha wakulima na wafugaji, wakulima na wananchi, serikali na wananchi, mwekezaji na mwananchi.

"Kasi ya serikali haioneshi kwamba migogoro itakwisha, tulitegemea serikali ingejipanga vizuri na kuongeza kasi kushughulikia matatizo hayo.

"Kama taifa bado hatuna mifumo bora ya kutatua changamoto za ardhi na hata wanaoongoza mabaraza ya ardhi, hawajapewa elimu ya kutosha ya namna ya kuitatua," alisema Dorothy.

Alisema chama chao kitakapoingia madarakani, kitahakikisha kinawashirikisha wananchi kikamilifu kupanga matumizi ya ardhi, ili kuepukana na migogoro ya kila siku.

Alisema wangeweza kutenga ardhi kutokana na mahitaji husika na kuondoa migogoro yote, lakini kuna suala la rushwa katika mabaraza ya ardhi ambako wanatamani migogoro inavyopelekwa huko itatuliwe.

Dorothy aliwaambia wananchi wa Kiteto kwamba, migogoro hiyo isipochukuliwa kwa umuhimu wake, athari yake ni kubwa na inaweza hata kusababisha mauaji.

"Chama chetu kina sera itakayomaliza changamoto hii, mojawapo ni kuondoa ardhi mikononi mwa Rais. Tutaweka katika mahakama inayotembea kutatua migogoro ya ardhi," alisema Dorothy.

Kiongozi wa chama huyo pia aliwaomba wananchi wa Kiteto kuchagua viongozi wanaotokana na chama hicho ili waje na mbinu mbadala alizoziita "za kukomboa nchi".

"Hatutakubali kilichotokea katika uchaguzi wa mwaka 2019 na 2020 kitokee tena awamu hii. Ni wajibu wenu kuchagua kiongozi tunayemtaka, lakini tunafahamu namna ambavyo kumekuwa na vitisho kwa viongozi wa upinzani ili turudi nyuma," alidai Dorothy.

Kukiwa na madai hayo ya rushwa kwa baadhi ya watendaji wa ardhi, juzi Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geophrey Pinda, akiwa mkoani Kilimanjaro, alionya watendaji wa ardhi wanaokiuka maadili, akisisitiza hakuna afisa ardhi atakayehamishwa eneo la kazi endapo akikiuka maadili ya utendaji wa taaluma yake.

# Mbarawa apongeza TPA ujenzi bandari mpya Mbamba Bay

**Na Mwandishi Wetu,** NYASA

WAZIRI wa Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, amepongeza Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA) kwa utekelezaji ujenzi wa bandari mpya na ya kisasa ya Mbamba Bay inayojengwa pembezoni mwa Ziwa Nyasa katika Wilaya ya Nyasa, mkoani Ruvuma.

Amesema ujenzi huo ni sehemu ya mkakati wa serikali kuboresha bandari mbalimbali nchini.

Akizungumza jana baada ya kutembelea eneo la mradi huo, Waziri Mbarawa alisema utasaidia usafirishaji haraka wa mizigo, zikiwamo bidhaa za viwandani, mazao ya kilimo na uvuvi, mizigo kwenda nchi jirani za Msumbiji, Malawi na Zambia zikitokea Bandari ya Mtwara kupitia Ziwa Nyasa.

"Ninapongeza sana TPA kwa ujenzi wa bandari hii ya aina yake kujengwa katika ukanda huu wa Ziwa Nyasa.

"Ujenzi huu mbali na kutoa ajira, pia utakuza uchumi wa nchi yetu na nchi za jirani zinazotumia bandari hii kusafirisha mizigo yao," alisema Waziri Mbarawa.

Alisema dhamira ya serikali ni kujenga miundombinu ya kisasa katika bandari zote ili kukuza uchumi na kutoa ajira kwa Watanzania.

Aliagiza TPA kusimamia vizuri ujenzi wa bandari hiyo kwa kushirikiana na mkandarasi mshauri wa mradi, ili umalizike katika muda uliopangwa na kuanza kutoa huduma.

Akitoa maelezo ya mradi huo kwa waziri, Mkurugenzi Msaidizi wa TPA, Juma Kijavara, alisema pamoja na mambo mengine, ujenzi wa bandari hiyo mpya ya kisasa utahusisha kujengwa gati mbili zenye urefu wa mita 103.

Alisema gati hizo zina uwezo wa kuhudumia meli mbili kubwa, tofauti na uwezo wa bandari ya sasa ambayo inahudumia boti ndogo za kubeba mizigo na abiria.

Kijavara alisema mradi huo utahusisha pia ujenzi wa maghala, nyumba za watumishi, jengo la utawala, jengo la abiria, karakana, mnara wa tangi la maji na jengo la huduma za afya.

Alisema kutakuwa na ujenzi wa daraja lenye urefu wa mita 105 na upana wa mita 15 kwa ajili ya magari ya kubebea mizigo na eneo la kuhifadhia makontena 3,000 ya mizigo.

"Pia tahusisha barabara za ndani na nje ya bandari kwa ajili ya magari kuingia na kutoka bandarini hapo," alisema.

Mhandisi wa mradi huo kutoka TPA, John Paul, alisema kuwa mpaka sasa utekelezaji mradi huo umefika asilima sita ambapo kazi zilizofanyika na zinazoendelea ni pamoja na usanifu wa kihandisi.

Alisema wanaendelea na maandalizi ya eneo la ujenzi ikiwa ni pamoja majengo ya ofisi za mkandarasi na mhandisi mshauri pamoja na kuleta vifaa na mitambo itakayotumika wakati wa ujenzi.

Paul alimweleza Waziri Mbarawa kuwa mpaka sasa, TPA imeshamlipa mkandarasi mjenzi malipo ya awali Sh. bilioni 3.2 sawa na asilimia tano na kumlipa mhandisi mshauri Sh. milioni 448.1, kama malipo ya awali ambayo ni sawa na asilimia 10.

Kwa mujibu wa taarifa ya TPA, kulinganisha na miaka ya nyuma, ujenzi wa bandari mpya utaongeza ufanisi, ikiwamo idadi ya shehena za mizigo na abiria wanaotumia Ziwa Nyasa.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa kwa kipindi cha miaka mitatu iliyopita (2021/22, 2022/23 na 2023/24), utendaji kazi wa bandari Ziwa Nyasa kwa ujumla umekuwa ukiongezeka ambapo kwa mwaka 2021/22, idadi ya mizigo ilikuwa tani 5,410 na idadi ya abiria ilikuwa 2,437. "Kwa mwaka 2022/23, idadi ya mizigo ilikuwa tani 11,351.40 na abiria walikuwa 70,172 na mwaka 2023/24 mizigo ilikuwa tani 2,619.56 na abiria walikuwa watu 15,194.

"Katika kipindi cha miaka mitatu, jumla ya mizigo yote iliyosafirishwa katika bandari hizo za Ziwa Nyasa ni tani 19,380.96 na abiria ni 87,803, huku tathmini ikionesha kuwa shehena kubwa ilitoka Bandari ya Mbamba Bay kulinganisha na Bandari ya Kiwira pamoja na nyingine za ukanda huo," inaonesha taarifa hiyo.

Kwa mujibu wa TPA, miongoni mwa faida za ujenzi wa bandari mpya ni kutoa fursa za ajira kwa vijana wanaozunguka mradi, fursa za biashara ikiwamo huduma ya chakula kwa mkandarasi na wafanyakazi na kukuza biashara na uchumi kikanda na kimataifa.

Taarifa hiyo ilisema bandari hiyo itaunganisha Tanzania na nchi jirani, kuhamasisha uwekezaji, hususan katika sekta ya viwanda na biashara.

"Ujenzi wa bandari hii mpya unasimamiwa na Mkandarasi Xiamen Ongoing Construction Group Limited na mshauri (Consultant) Anova Consult na unatarajiwa kukamilika Januari 26, 2026," inabainisha taarifa hiyo.

# Wawili wauawa kisha miili yao kuchomwa moto tuhuma wizi

**Na Vitus Audax**

WATU wawili wakazi wa Mtaa wa Buzunza, mkoani Simiyu, wanadaiwa kupigwa hadi kufariki dunia kisha miili yao kuteketezwa kwa moto wakituhumiwa kukutwa na mali zinazodhaniwa za wizi.

Wawili hao ni Ntawa Limbu (32) ambaye ni mkulima pamoja na mwenzake aliyetambulika kwa jina moja la Suma, wote ni wakazi wa Mtaa wa Buzunza, mkoani humo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Simiyu, Edith Swebe, alithibitisha jana kutokea kwa tukio hilo na kwamba wanawashikilia watu watano kwa tuhuma za mauaji hayo.

Alisema watu hao wanatuhumiwa kujichukulia sheria mkononi kwa kuwakamata na kuwaua watu wawili kisha kuteketeza miili yao kwa moto.

"Chanzo cha kufanya uhalifu huo wa kujichukulia sheria mkononi ni kwamba, inasemekana wawili hao walikuwa wanamiliki mali zinazosadikika kuwa za wizi na mara baada ya taarifa kumfikia aliyewahi kuibiwa, alihamasisha kundi la vijana waendesha bodaboda na kuanza kuwatafuta watuhumiwa ambao kwa sasa ni marehemu," alisema.

Kamanda Edith alisema Jeshi la Polisi linakamilisha uchunguzi ili taratibu zingine za kisheria zifuate ikiwa ni pamoja na kuwafikisha mahakamani watuhumiwa hao.

"Tunaendelea kutoa wito kwa wananchi kuacha tabia za kujichukulia sheria mkononi kwani ni kosa kisheria, Jeshi la Polisi litawakamata na kuwafikisha mahakamani," alisema Kamanda Ed-



Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu (katikati), akipokea sehemu ya msaada wa vyandarua 337 na mashuka 350 kutoka kwa Meneja wa Benki ya Stanbic Tanzania tawi la Moshi, Hoboka Mwamakunge, Mjini Moshi jana, kwa ajili ya Hospitali ya Rufani ya Mawenzi, ikiwa ni mipango endelevu ya benki hiyo katika kuboresha sekta ya afya katika jamii yetu. Kulia ni Kaimu Mganga Mkuu wa hospitali hiyo, Dk. Jonas Kessy. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Pinda aonya maofisa ardhi wanaokiuka maadili

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geophrey Pinda amesema hakuna ofisa ardhi atakayehamishwa eneo la kazi endapo akikiuka maadili ya utendaji wa taaluma yake.

Alitoa onyo hilo juzi wakati mkutano wa pamoja wa wananchi na watumishi wa ardhi uliofanyika katika ukumbi wa mikutano wa Mkoa wa Kilimanjaro.

"Nikimwambia Katibu Mkuu huyu utendaji kazi wake unaripotiwa kwamba hafai, tutatuma vyombo vitakuja kukutafakari upya.

"Usikubali dawati lako liwe chanzo cha mgogoro, upelekwe kwa Mkuu wa Wilaya, kwa Mkurugenzi, kwa mbunge na jamno lile uliloanzisha wewe linakwenda mpaka kwa Rais. Haiwezekani! Kila mtu ajitafakari," alionya Pinda.

Naibu Waziri huyo pia alitoa maelekezo kwa Ofisi za Wasajili wa Hati nchini kuharakakisha mchakato wa utoaji hatimiliki za ardhi ili wananchi waweze kunufaika nazo ikiwa pamoja na kuaminiwa kupata mikopo katika taasisi za kifedha.

"Maelekezo ninayoyatoa kwenye dawati la usajili usilaze kazi, toeni hati ziende kwa wananchi," aliagiza Naibu Waziri Pinda.

Kiongozi huyo pia aliwaonya maofisa ardhi wanaojiuhusisha na ugawaji kiwanja kimoja mara mbili na kusisitiza kuwa wizara yake itachukua hatua kali za kinidhamu dhidi ya mtumishi yeyote atakayekiuka maadili ya utumishi wa umma kwa taaluma yake.

"Kama litamhusisha ofisa wa kwetu kwenye jambo la kugawa kiwanja kimoja mara mbili, sasa hivi hatunamswalia Mtume, tutachukua hatua kali," alionya.

Naibu Waziri Pinda alihitimisha ziara yake mkoani Kilimanjaro jana, ambako mbali mambo mengine, alisikiliza na kutatua changamoto za ardhi kwa wananchi wa mkoa huo pamoja na kufanya vikao kazi na watumishi wa ardhi mkoani humo.

# TEMESA yatakiwa kuboresha ukusanyaji mapato

**Na Neema Macha**

NAIBU Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Dk. Charles Msonde, ameelekeza Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania kuboresha mikakati ya ukusanyaji mapato kwenye vituo vyake nchini ili kuongeza uwezo wa kifedha wa wakala katika kufanikisha miradi zaidi ili kufikia malengo yaliyokusudiwa. Dk. Msonde aliyasema hayo alipotembelea TEMESA mkoani Dar es Salaam hivi karibuni, kufuatia maagizo ya Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa ya kumtaka kufuatilia utendaji wa wakala na kuhakikisha kuwa miradi inatekelezwa kwa viwango vya hali ya juu.

Katika ziara yake, Dk. Msonde aliagiza TEMESA kutafuta mbinu mpya na za kisasa katika ukusanyaji mapato huku akisisitiza kuwa mifumo bora itasaidia kuimarisha huduma zinazotolewa kwa wateja na taasisi itaweza kujiridhisha na matumizi ya uendeshaji vivuko.

"Ni muhimu kuhakikisha kuwa kila shilingi inayokusanywa inatumika ipasavyo kwa ajili ya maendeleo ya wakala na wananchi, hii ni fursa nzuri kwa TEMESA kuonesha ufanisi wake na kujenga uaminifu kwa wananchi. "Tunatarajia kuona mabadiliko chanya katika ukusanyaji mapato na huduma zinazotolewa," aliongeza Dk. Msonde.

Akizungumza na viongozi na wahandisi wa TEMESA, Dk. Msonde alisisitiza umuhimu wa utekelezaji mzuri wa kazi ili kukidhi mahitaji ya jamii.

Aliagiza viongozi wa vituo vyote nchini kujifunza kutokana na mbinu na mikakati inayotumika katika vituo vya Dar es Salaam, akisema kuwa ni fursa muhimu kwa maendeleo ya sekta ya ufundi na umeme.

"Nimeongea na baadhi ya madereva na taasisi mbalimbali zinazohudumiwa na TEMESA hapa Dar es Salaam, hasa katika utengenezaji magari na taasisi hizo zimeonesha kuridhishwa na huduma zinazotolewa na TEMESA," alisema Dk. Msonde.

Aliongeza, "Huduma kwa wateja ni nzuri zaidi, ukaguzi wa magari unafanyika haraka. Ni muhimu kuwapongeza watendaji wetu, hasa katika Kanda hii ya Dar es Salaam kwa kuboresha utendaji wao wa kazi na nitoe wito kwa mikoa yote nchini kuiga utendaji bora wa TEMESA Dar es Salaam."

Dk. Msonde pia alipongeza TEMESA na kutaka wakala huo utafute ufumbuzi wa haraka kwa changamoto zinazoukabili.

Kiongozi huyo pia pia aliwaagiza watendaji wote kuzingatia ubora katika huduma ili kukidhi mahitaji ya wananchi na kuimarisha ufanisi wa shughuli zao.

Alisema ziara hiyo ni sehemu ya mikakati ya serikali katika kuhakikisha sekta ya ujenzi, uendeshaji na huduma za umeme vinaimarishwa kwa faida ya wananchi wote.

# LATRA yarejesha barabarani mabasi sita ya Katarama

**Na Elizabeth Zaya**

MAMLAKA ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imeruhusu mabasi sita kati ya 10 ya kampuni ya Katarama kuanza kufanya kazi.

Wiki iliyopita LATRA ilisitisha kwa muda usiojulikana leseni ya utoaji huduma kwa mabasi yote ya kampuni hiyo kuanzia Septemba 13 mwaka huu kutokana na ukiukaji sheria, kanuni na taratibu za usafirishaji, ikiwamo kuchezea mifumo ya udhibiti wa mwendokasi.

Baada ya kusitisha huduma kwa mabasi ya kampuni hiyo, LATRA kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi, walianza kufanya uchunguzi.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano wa LATRA, Salum Pazzy, alisema kuwa baada ya kufanyika uchunguzi wa awali, wamebaini kwamba kati ya mabasi 10, manne ndio yalibainika kuchezea mfumo.

"LATRA pamoja na kudhibiti, kisheria pia imepewa mamlaka ya kuwalea wasafirishaji kuhakikisha biashara yao inalindwa na wakaendelea kustawi kwa ajili ya kutoa huduma. Kuliko kuendelea kusimamisha mabasi yote, iliona bora itoe rukhsa hayo sita ambayo hayakufanya makosa.

"Lakini kabla ya hapo, iliita uongozi wa mabasi hayo kuwapatia masharti kabla ya kuwaruhu na wakaahidi kutekeleza, hivyo tunaamini kwamba wakati haya mengine manne yanayoendelea kuchunguzwa, hayo yaliyoruhusiwa yatafanya vizuri kwa sababu kama mamlaka hatuko tayari kuona maisha ya Watanzania wanaotumia huduma yao yanakuwa hatarini," alisema.

Baadhi ya makosa ambayo yalibainika kufanywa na mabasi hayo ni pamoja na kuondoa kifaa kilichofungwa na LATRA katika mabasi na kufanya ujanja wa kufunga kifaa chao kingine cha kutuma taarifa zisizo sahihi kwa Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS).

"Pia yalibainika kufanya vurugu barabarani kwa mwendo kasi na kung'oa sehemu ya kifaa kinachotuma taarifa ya mwenendo wa mabasi na kubadilisha kifaa cha antena na hivyo kutuma taarifa zisizo sahihi kwa mamlaka," alisema.

Pazzy alisema mamlaka inaendelea kufuatilia mabasi yote yanayovunja sheria na haitosita kuchukua hatua kwa wasafirishaji wote wanaokiuka sheria na taratibu za usafirishaji.



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Balozi Dk. John Simbachawene (kushoto), akiangalia bidhaa ya nguo iliyotengenezwa na Mkurugenzi wa Beta More Production, Tatu Mpogo (kulia), wakati wa uzinduzi wa Siku ya Viwanda Vidogo na Wazalishaji wadogo Tanzania, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# 21 wakamatwa kwa tuhuma za mauaji

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

JESHI la Polisi Mkoa wa Singida linawashikilia watu 21 kwa tuhuma za makosa mbalimbali ya mauaji.

Kati yao, 13 wameunganishwa katika kesi ya mauaji inayomkabili mganga wa kienyeji aliyetuhumiwa kuua watu 10 na kuwazika katika makazi yake. Mganga huyo, Kamba Kasubi, anadaiwa kuua watu hao na kuwazika katika makazi yake kijijini Makuro, wilayani Singida na katika Kijiji cha Porobanguma, wilayani Nchemba, mkoani Dodoma kwa nyakati tofauti.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Singida, Mayunga Mayunga, akizungumza na waandishi wa habari juzi mjini hapa, alisema kuwa katika kipindi cha Julai hadi Agosti mwaka huu, jeshi hilo limewakamata watuhumiwa 137 wa makosa mbalimbali katika doria na misako ya kubaini, kuzuia na kutanzua uhalifu.

"Watuhumiwa hao wamekamatwa baada ya kutenda makosa tofauti yakiwamo makosa ya mauaji (watuhumiwa 21), watuhumiwa 34 kwa kukutwa na pikipiki zinazodhaniwa kuwa ni za wizi na watuhumiwa 21 wa dawa za kulevya aina ya bangi gramu 8,773," alisema.

Kaimu Kamanda Mayunga alisema watuhumiwa wengine wanne walikamatwa na dawa za kulevya aina ya mirungi zenye uzito wa gramu 19,842, mmoja akiwa dawa aina ya Heroin uzito wa gramu 0.5, wakati wengine 15 walikutwa na pombe haramu ya moshi lita 78.

Aliongeza kuwa watuhumiwa watano walikamatwa kwa makosa ya kubaka, watatu kwa tuhuma za wizi wa kompyuta, watano kwa tuhuma za wizi wa simu ndogo, wanne kwa tuhuma za wizi wa mitungi midogo ya gesi, mmoja kwa wizi wa TV mbili na wengine walikamatwa kwa tuhuma za wizi wa redio, mifugo huku watatu wakidaiwa kukutwa na nyara za serikali.

"Jeshi la Polisi linawashukuru wananchi kwa kuendelea kutoa ushirikiano katika kubaini na kuzuia uhalifu na linawaomba kufika mahakamani kutoa ushahidi ili kesi za mauaji hayo ziweze kupata mafanikio," alisema.

# Serikali kujenga shule za ufundi 100

**Na Elizabeth John, NJOMBE**

SERIKALI inajenga shule za sekondari za ufundi 100 nchi nzima ili kuwaandaa vijana kupambana katika sekta ya ajira.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, alibainisha hayo wakati akizungumza na viongozi mbalimbali wa serikali mkoani Njombe.

Alisema kuwa kwa mkoa wa Njombe, shule hiyo maalum ya sekondari itajengwa eneo lililotengwa katika Kijiji cha Magoda lenye ukubwa wa ekari 26.

Prof. Mkenda alisema serikali imeanzisha miradi, ikiwamo kwenye sekta za afya, elimu na maji ambako kote fedha zimekwenda ili kuikamilisha na kuwaondolea adha wananchi.

"Kuna barabara, bado tumepewa fursa ya kujenga shule amali za mrengo wa ufundi kwa sababu amali ni ufundi na ufundi stadi," alisema Prof. Mkenda.

Waziri huyo aliwataka watumishi wa serikali mkoani humo kutoona haya kueleza mafanikio ya serikali katika utekelezaji miradi ya maendeleo.

"Rais huyu (Samia Suluhu Hassan) tunajua ameanza kuingia makubaliano ya kurudisha hadhi ya reli ya Tazara ifanye kazi kama inavyotakiwa, tuanze kulima vizuri maparachichi kwa sababu miundombinu imeboreshwa," alisema Prof. Mkenda.

Alisema kuwa hivi sasa serikali itahakikisha kila mtoto anakwenda shule ya sekondari na msingi kwa sababu hakuna ada na itaendelea kuboresha miundombinu kuwa ya kisasa.

Katibu Tawala Mkoa wa Njombe, Judica Omari alisema kuwa katika sekta ya elimu, mkoa huo umepokea Sh. bilioni 58.4 kwa ajili ya uwezeshaji huduma za elimu ukiwamo ujenzi wa miundombinu ya madarasa na mabweni.

Mbunge wa Njombe Mjini, Deo Mwanyika alisema serikali imeleta fedha kwa ajili ya ujenzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo, ikiwamo ya sekta ya maji.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mashabiki nchini zipeni nguvu Simba, Yanga michuano CAF

**VIGOGO** wa kandanda nchini, Simba na Yanga zote kutoka jijiji, Dar es Salaamzinatarajia kupeperusha bendera ya Tanzania katika mashindano ya kimataifa yanayoandaliwa na kusimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga wao wanashuka kwenye uwanja wa Amaan Complex Zanzibar kuwakaribisha CBE kutoka Ethiopia katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika wakiwa na kumbukumbu ya ushindi wa bao 1-0 wakati Wekundu wa Msimbazi wao watawakabili Al Ahly Tripoli kutoka Libya kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho, mechi ya kwanza wakitoka suluhu.

Wawakilishi hao pekee wa Tanzania waliobakia katika mashindano ya kimataifa walianzia ugenini na wikendi hii watamalizia vibarua hapa nyumbani, Yanga wakicheza leo huko Visiwani Zanzibar na Simba yenyewe itakuwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa hapo kesho.

Kwa namna mpira wa miguu ulivyo sasa, hakuna timu ambayo unaweza kusema iko katika nafasi nzuri ya kusonga mbele kutinga hatua ya makundi, wawakilishi hawa wawili wanatakiwa wafahamu bado wana jukumu la kwenda kupambana kusaka ushindi wa aina yoyote ili kusonga mbele katika mashindano hayo ya CAF yanayofanyika kila mwaka.

Simba na Yanga hawatakiwi kuwadharau wapinzani wao kwa sababu yoyote ile, wasiwe na mawazo kwamba wao majina yao ni makubwa au wanajivunia wanacheza kwenye ardhi ya nyumbani kwa Mama Samia Suluhu Hassan na Dk. Hussein Mwinyi.

Wachezaji wetu wa Simba na Yanga wanatakiwa kuingia uwanjani wakifahamu wamebeba furaha ya Watanzania na wanatakiwa kuilinda kwa 'Jasho na Damu' na si vinginevyo.

Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi na Kocha Mkuu wa Simba, Fadlu Davis, wanatakiwa kukamilisha vyema tathmini na kupanga wachezaji ambao wataingia uwanjani kusaka ushindi huku wakitumia mapungufu ya wapinzani ambayo waliyabaini katika michezo ya awali na hatimaye kujiweka kwenye nafasi nzuri ya kusonga mbele.

Viongozi wa Simba na Yanga, huu ni wakati mwingine muhimu wa kutimiza majukumu yenu kwa kufanya kila kinachotakiwa na kinachowezekana ili kupata ushindi na hatimaye kutinga hatua ya makundi huku Azam FC na Coastal Union ambazo zimetolewa na timu nyingine za Tanzania kuendelea kujifunza namna ya kupambana kimataifa.

Tunahitaji kuona viongozi wanazidisha umoja na ushirikiano bila kuwaweka pembeni 'wakubwa' wa soka Tanzania (TFF), katika kuhakikisha ushindi unapatikana na malengo ya kutinga hatua ya makundi kwa mara nyingine yanatimia.


Lakini ili haya yote yatimie, huu ni wakati muhimu kwa mashabiki wote wa soka Tanzania kuungana pamoja katika kutoa sapoti kuwashangilia wachezaji wetu wa Simba na Yanga wanapokuwa dimbani wakipeperusha bendera ya nchi katika mashindano hayo ya kimataifa. Mashabiki ni sawa na mchezaji wa 12 uwanjani, hawa ni kiungo muhimu katika kufikia malengo ya timu iwe klabu au timu ya taifa, mashabiki wanatakuwa kuwa kitu kimoja kwa sababu kufanya vyema kwa timu zote mbili, kutaipa Tanzania nafasi ya kutoa wawakilishi wanne kwenye michuano hiyo ya CAF.

Umefika wakati ile tabia ya kuwapa ushirikiano wapinzani na kutoa 'siri' ili upande wa pili ufungwe, usichukue nafasi kwa maslahi makubwa ya nchi na si jambo lingine lolote.

Tanzania inahitaji kuendelea kupeperusha bendera yake katika mashindano hayo huku tukiwa na kiu ya kuliona taji la Ligi ya Mabingwa Afrika au Kombe la Shirikisho Afrika linatua nchini, na ili tufike huku ni lazima tuonyeshe mabadiliko kwa kushangilia wachezaji wetu na kuweka pembeni ushindani wetu uliopo tunapokutana kwenye mechi za Ligi Kuu Bara.

**Kila la heri Yanga, kila la heri Simba katika mechi za CAF.**

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Wachezaji wa CHAN waanze kuangaliwa sasa

**TAYARI** Shirikisho la Soka Afrika (CAF) limetangaza tarehe za Fainali za Mataifa ya Afrika kwa wachezaji wa ndani (CHAN) 2025, itakayofanyika Tanzania, Kenya na Uganda.

Makamu wa 4 wa Rais wa CAF, Seidou Mbombo Njoya, ambaye pia anahudumu kama Mwenyekiti wa kamati ya maandalizi ya Michuano ya Mataifa ya Afrika (CHAN) ndiye aliyetamka rasmi, Jumatatu iliyopita, mchana wakati wa mkutano na waandishi wa habari baada ya kikao cha Kamati ya Utendaji ya CAF jijini Nairobi nchini Kenya.

Itafanyika Februari 1 hadi 28 nchini Kenya, Uganda na Tanzania. Pia ilithibitishwa kuwa mechi za kufuzu kwa CHAN zitaanza kati ya Oktoba 25-27 na kumalizika Desemba mwaka huu kabla ya fainali hizo.

Nchini Tanzania serikali inaonekana kujiandaa kwa vitendo kwani tayari imeanza kujiandaa kwa miundombinu kwa kujenga viwanja vipya, kukarabati vilivyopo, kukarabati na baadhi ya viwanja ambavyo vitatumika kwa mazoezi.

Pamoja na baadhi ya viongozi wa serikali kuzungumzia hilo, Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Damas Ndumbaro, na naibu wake Hamisi Mwinjuma, lakini hata kwa macho vitendo vinaonekana kuwa nchi inapambana kwa ajili hiyo.

Na hii ya CHAN ni kama majaribio ya michuano ya AFCON ambayo Tanzania ni mwenyeji wake 2027, kwa ushirikiano wa Kenya na Uganda.

CAF wamezipa nchi hizi CHAN, ikiwa ni kama majaribio ya AFCON, ambayo huchezwa na wachezaji wote wanaocheza ndani na nje ya nchi.

Wakati serikali ikipambana, upande wa ufundi nao inabidi upambane kuangalia wachezaji bora ambao wanaweza kuiwakilisha nchi katika michuano ya CHAN.

**Pamoja na baadhi ya viongozi wa serikali kuzungumzia hilo, Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Damas Ndumbaro, na naibu wake Hamisi Mwinjuma, lakini hata kwa macho vitendo vinaonekana kuwa nchi inapambana kwa ajili hiyo.**

Kwa sababu CHAN ni michuano ya wachezaji wa ndani, ina maana inawashirikisha wachezaji wale tu wanaocheza Ligi Kuu Tanzania Bara, au Championship.

Ushauri wangu ni kwamba Shirikisho la Mpira wa Miguu Nchini (TFF), linatakiwa kuwawezesha makocha wa timu za taifa, Hemed Suleiman 'Morocco' na mwenzake Juma Mgunda kuzunguka nchi nzima kuangalia michezo mbalimbali ya Ligi Kuu ili kuangalia wachezaji watakaokuwa kwenye kikosi hicho.

Pamoja na kwamba klabu za Simba, Yanga na Azam wana wachezaji wa Kitanzania bora, lakini tusiendelee kukariri kwamba katika klabu zingine hakuna wachezaji wazuri.

Kwa sababu michuano ya CHAN haiwahusu wachezaji wa nje, kuwe na wigo wa kuwapata wachezaji wengine bora kutoka klabu zingine.

Ukitaka kujua wachezaji wazuri wapo, ila kuna tatizo la kuwatambua, kila msimu klabu za Simba na Yanga zinasajili kutoka klabu hizo hizo za chini. Wakati mwingine mpaka zile timu ambazo zimeshuka daraja.

Sasa unashangaa Kamati za Ufundi za TFF inashindwa vipi kuwawezesha makocha wake kusaka wachezaji wengine wazuri mikoani kutoka klabu mbalimbali nchini badala ya kujaza wa Simba na Yanga na Azam tu kwenye kikosi.

Februari mwakani si mbali, hivyo kazi hiyo ianze sasa. wakati serikali inaendelea na mchakato wa viwanja na miundombinu, TFF nayo ianze kazi ya kuanndaa wachezaji kwa kuwaangalia wanaofaa kuchezea timu ya taifa kwenye michuano ya CHAN, wakati Ligi Kuu Tanzania Bara inaendelea.

# Ulega awataka wafugaji kufuata sheria

Na Mwandishi Wetu

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, amewataka wafugaji kuishi kwa amani na kuheshimu sheria za nchi ikiwamo kuacha tabia ya kuingiza na kulisha mifugo yao katika mashamba ya wakulima.

Waziri Ulega alisema hayo wakati wa kikao cha kusikiliza kero na changamoto za wafugaji wa Wilaya ya Namtumbo, kilichofanyika wilayani humo Septemba 19.

"Wafugaji muishi na watu vizuri, acheni ubabe, fuateni sheria, msiingize mifugo katika mashamba ya watu kwa makusudi, ni jambo baya sana, msipofuata sheria kila mtu mtamuona mbaya," alisema.

Aidha, aliwataka wafugaji hao kuunda mabaraza ya wazee ya wafugaji ili yasaidie kusuluhisha migogoro na kukemea wachache wanaotaka kuharibu taswira ya ufugaji nchini.

Aliwahimiza wafugaji hao kuweka utaratibu wa kuvuna mifugo yao na kuiuza, kwa kuwa kutawasaidia kujipatia kipato na pia kupunguza wingi wa mifugo ili kujiepusha na migogoro baina yao na watumiaji wengine wa ardhi.

Katika hatua nyingine, Waziri Ulega amewaelekeza wataalamu kutoka wizarani kwake kwenda kutoa elimu ya ufugaji bora na fursa zilizopo kwenye ufugaji kwa viongozi, wafugaji na makundi mengine katika wilaya hiyo ili wajue umuhimu wa uchumi ju-




Baadhi ya wafugaji wakimsikiliza Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega (hayupo pichani) wakati wa kikao chake cha kusikiliza kero na changamoto zao katika wilaya ya Namtumbo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kafulila akoshwa ujenzi mabweni kwa PPP

Na Joseph Mwendapole

KAMISHNA wa Ubia Kati ya Sekta ya Umma na Binafsi (PPP), David Kafulila, amevitaka vyuo nchini kuiga mfano wa Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) kujenga mabweni kwa ubia bila kutegemea fedha za serikali.

Amesema miradi ya ubia inanufaisha zaidi serikali kwa kuwa inapata teknolojia mpya na za kisasa kutoka sekta binafsi na kusaidia uchumi wake kuendeshwa kisasa zaidi na kwa ufanisi.

Aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati anazungumza kwenye mkutano wa wadau wa chuo hicho kilichojadili utekelezaji mradi wa ubia wa ujenzi wa mabweni yatakayokuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 12,000.

"CBE imeonesha njia, imetengeneza mwongozo ambao vyuo vingine vinapaswa kuiga kwa kujenga mabweni kwa ubia bila kuomba Hazina fedha za uendeshaji," alisema Kafulila.

Alisema mamlaka zote za serikali zinazotekeleza miradi mbalimbali, ziangalie uwezekano wa kuhusisha sekta binafsi kwenye utekelezaji miradi hiyo badala ya kusubiri fedha za serikali.

Alisema kila mradi ambao sekta binafsi inaweza kuutekeleza ni vyema taasisi za serikali zikaingia ubia ili kuharakisha utekelezaji wake na kuokoa fedha za serikali ambazo zingetumika.

"Kila mradi ambao sekta binafsi inaweza kuutekeleza kwa teknolojia ya hali ya juu kuliko serikali, basi apewe autekeleze ili tujenge uchumi wa kisasa ambao sekta binafsi ndiyo ina nafasi kubwa ya kutengeneza ajira nyingi," alisema.

Alipongeza Menejimenti ya CBE kwa kuratibu mradi wa ujenzi wa mabweni hayo ambayo yatakapokamilika yataondoa uhaba wa malazi kwa wanafunzi kwenye kampasi ya chuo hicho jijini Dar es Salaam.

Kafulila alisema serikali iliamua kuweka utaratibu wa kuweka miradi kwa ubia ili kunufaika na mambo manne, ikiwamo kutekeleza miradi yake bila kutumia fedha zake au mikopo kutoka mataifa ya nje.

"Utaratibu wa ubia unaleta unafuu kwa serikali kwa sababu miradi inajengwa bila kutegemea fedha zake, utaratibu huu wa ubia pia unafanya serikali ivute teknolojia ya kujenga baadhi ya miradi, teknolojia ambayo kwa kiasi kikubwa inapatikana sekta binafsi," alisema.

Alisema kwa utaratibu wa ubia serikali inanufaika na teknolojia ya kisasa ambayo inapatikana kwenye sekta binafsi na kupata fursa ya kuleta weledi kwenye taasisi zake kama CBE.

"Kwa mfano, mabweni haya yatakapojengwa na kukamilika, mwekezaji atalipa kodi kwa serikali lakini kama ingejenga yenyewe, ingekuwa huduma tu na hakuna kodi ambayo serikali ingepata, hivyo utaratibu huu unainufaisha sana serikali," alisema.

Mkuu wa chuo hicho, Prof. Edda Lwoga, alisema kushirikiana na Kituo cha Ubia wa Sekta za Umma na Binafsi (PPP) wanatatarajia kujenga mabweni ya wanafunzi kwa ubia utakaogharimu Sh. bilioni 20.7.

Alisema mabweni hayo yatakayojengwa kwenye kampasi kuu ya Dar es Salaam, yatakuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 12,728, hivyo kupunguza pengo kubwa la malazi kwa wanafunzi.

Alisema kuwa hivi sasa kampasi ya CBE Dar es Salaam ina jumla ya wanafunzi 12,000, ambapo kwa upande wa malazi, kampasi ina majengo mawili tu ya bweni yenye uwezo wa kuchukua vitanda 160 pekee vya malazi kwa wanafunzi wa kike na kiume, hivyo vinakidhi uhitaji wa malazi kwa asilimia 1.3 tu.

Mkuu wa chuo alisema mradi huo utakapokamilika unatarajiwa kupunguza changamoto ya malazi kutoka asilimia 1.34 iliyopo mpaka asilimia 30 ya mahitaji ya wanafunzi kwa bweni.

"Hali iyopo imesababisha uhitaji mkubwa wa malazi ya wanafunzi kwa asilimia 98.6, hivyo wengi wanalazimika kutafuta malazi nje ya chuo kwa gharama kubwa, jambo linalosababisha baadhi ya wanafunzi kushindwa kumudu gharama hizo," alisema.

## KABWELA — Na Fadhili Mohammed



# Atiwa mbaroni kwa tuhuma za kumtoboa macho mtalaka wake

**Na Waandishi Wetu**

JESHI la Polisi mkoani Shinyanga linamshikilia Paulo Shija (19), mkazi wa Kata ya Ndala, Manispaa ya Shinyanga kwa tuhuma za kumjeruhi na kumtoboa macho yote mtalaka wake, Ester Mataranga (25), mkazi wa Ndala.

Akithibitisha kukamatwa kwa mtuhumiwa huyo, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, SACP Janeth Magomi alisema walipokea taarifa ya tukio hilo Agosti 13 mwaka huu kuwa Shija alimtoboa macho yote mawili kisha kutokomea kusikojulikana.

"Baada ya kupokea taarifa hiyo, tulifika eneo la tukio na kumchukua majeruhi huyo na kumpeleka katika Hospitali ya Kolandoto iliyoko Halmashauri ya Kishapu kwa ajili ya kupewa matibabu," alisema SACP Magomi.

Alisema kuwa baada ya hatua hiyo, jeshi hilo liliendelea kumtafuta mtuhumiwa huyo kwa kushirikiana na wananchi na kufanikiwa kumtia mbaroni Septemba 17 mwaka huu.

"Tulimkamata akiwa maeneo ya Masekelo, Manispaa ya Shinyanga na kumfikisha kituoni kwa taratibu zaidi za kisheria na upelelezi ukikamilika atafikishwa mahakamani. Tunakemea vikali wananchi wote wanaojichukulia sheria mkononi," alisema Kamanda.

Akizungumza na Nipashe hospitalini hivi karibuni, Ester (25) alidai kutobolewa macho na mtalaka wake huyo (Shija), wakati wakielekea kwenye nyumba walikokuwa wanaishi awali kwenda kuchukua mizigo yake na talaka iliyokuwa imeandaliwa baada ya mtalaka wake kuoa mwanamke mwingine.

Alisema kuwa tukio hilo lilitokea Agosti 13 mwaka huu saa 12 asubuhi na kuwa awali walikuwa wanaishi vyema katika ndoa yao na walibahatika kupata watoto wawili, lakini baadaye walikorofishana kutokana na kile alichodai "wivu wa mapenzi".

Alidai kuwa mtalaka wake huyo alikuwa akimtuhumu kutoka nje ya ndoa na kulazimika kurejea nyumbani kwao katika Kijiji cha Kundikiria-Ukeme na kuendelea na maisha mengine pamoja na wazazi wake. Ester alidai kuwa akiwa nyumbani kwa wazazi wake, walikuwa wakiwasiliana mara kwa mara na Shija kumwomba arejee Ndala walikokuwa wanaishi kwenda kuchukua mizigo yake baada ya mtalaka wake huyo kuoa mwanamke mwingine.

"Nilianza safari Agosti 10 kwenda kuchukua mizigo na talaka pia. Siku ya Jumapili ya tarehe 11 Agosti, nilimpigia simu mtalaka wangu na kumwambia ningefika Ndala tarehe 12 Agosti mwaka huu na tulikubaliana na nilipofika Kituo cha Mabasi Shinyanga (Manyoni), alinipokea vyema.

"Nilipatiwa chakula na kupelekwa nyumba ya kulala wageni kwa ajili ya kupumzika kusubiria siku iliyokuwa inafuata tuelekee nyumbani," alidai. Ester anaendelea kusimulia kuwa siku hiyo walilala pamoja na ilipotimu saa 10 alfajiri ya tarehe 13 Agosti, mtalaka wake huyo alimlazimisha waondoke lakini alikataa kwa maelezo kuwa aliona ilikuwa usiku sana na ilipotimu saa 12 asubuhi walitoka na kungozana pamoja.

"Tulipofika sehemu ya kichaka, barabara ya Musoma Food, mtalaka wangu alidai anataka kujisaidia haja ndogo. Mimi nikatangulia mbele, ghafla nikakabwa.

"Alinivuta kwa nguvu kanga niliyokuwa nimejitanda shingoni. Nikaanza kukimbia huku nikipiga kelele kuomba msaada.

"Baada ya kuona viashiria vibaya, alinikaba shingo na kuishiwa nguvu na kuanguka chini na alijua ameniua na kunitoa macho. Nimekuja kushtuka niko hospitalini nikipatiwa matibabu," alidai Ester.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Kolandoto aliyempokea mgonjwa na kuanza kumpatia matibabu, Dk. Wallace Sahani alisema Ester ametobolewa macho yote, lakini jicho moja limeharibika kabisa na lingine linahitaji matibabu ya kibingwa na wanataraja kumpatia rufani apelekwe katika Hospitali ya Kanda ya KCMC, mkoani Kilimanjaro.

"Jicho lake moja halioni vizuri, kuna damu imevujia ndani, hivyo talazimika kumpatia rufani akapate matibabu ya kibingwa ili aweze kuona vizuri, kwani alifika akiwa na hali mbaya akiwa na majeraha makubwa lakini kwa sasa tumeyaweka sawa," alisema Dk. Sahani.

***Imeandaliwa na Vitus Audax na Shaban Njia**



Naibu Mkurugenzi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), Juma Kajavara (katikati) akitoa maelezo ya ufafanuzi wa ramani ya ujenzi wa bandari mpya ya Mbamba Bay, wilayani Nyasa, mkoani Ruvuma kwa Waziri wa Uchukuzi Prof. Makame Mbarawa (kulia), alipofanya ziara bandarini hapo, jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# 'Wanaohamasisha mmomonyoko wa maadili mtandaoni washughulikiwe'

**Na Elizabeth Zaya**

WAZIRI wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Damas Ndumbaro ameagiza Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kuwashughulikia wale wote wanaohamasisha mmomonyoko wa maadili kupitia mitandao ya kijamii na kusigina mila na tamaduni za kitanzania.

Dk. Ndumbaro alielekeza kuchukuliwa hatua hiyo jana wakati akifungua Tamasha la Kitaifa la Utamaduni mjini Songea, mkoani Ruvuma lililobebwa na kaulimbiu 'Utamaduni wetu ni utu wetu, tuuenzi na kuuendeleza.'

Alisema hakuna taifa lolote duniani lisiloheshimu na kuthamini mila, desturi na tamaduni zao na kwamba ni jukumu la TCRA kuwashughulikia ipasavyo wale wote wanaotumia vibaya mitandao hiyo. "TCRA mna jukumu kubwa la kuhahikisha wale wanaokiuka mila na desturi za kitanzania, kuzisigina na kuhamasisha mambo yanayochangia kuleta mmomonyoko wa maadili katika nchi yetu wanashughulikiwa ipasavyo.

"Tusipokuwa na utamaduni wetu, hatuna utu na tusipouenzi, hatutauendeleza na ili taifa liwe hai, lazima kuenzi na kuendeleza utamaduni wake, lazima turithishe utamaduni kwa watoto na vijana.

"Tuwafundishe mila na desturi za kitanzania, Lugha ya Kiswahili, miiko yetu na ndipo taifa litaendelea kuwa hai," alisema.

Dk. Ndumbaro alisema wapo baadhi ya watu wamekuwa wanatumia vibaya tafsiri ya haki za binadamu kuingiza tamaduni za kigeni ambazo ni kinyume cha zile za kitanzania, akisisitiza kuwa suala hilo halikubaliki.

"Haki za binadamu ni suala muhimu sana ambalo tunahitaji kuliheshimu na kulizingatia, lakini baadhi tunatumia haki za binadamu vibaya kwa kuingiza tamaduni za kigeni zisizofaa katika jamii yetu.

"Tusitumie kisingizio hicho kukiuka miiko, maadili na desturi zetu kwa kuwa tukifanya hivyo tutakuwa tunaua nchi yetu, nchi yetu itakuwa mfu.

"Waswahili wanasema 'mkataa kwao ni mtumwa na sisi tusikatae kwetu'. Katika kuenzi mila na desturi, lazima tutambue taasisi muhimu ambazo zinaweza kufanikisha jambo hilo, tukianza na familia, taasisi za dini, vyombo vya habari, shule na nyinginezo," alisema.

Dk. Ndumbaro alisema maadili mazuri ndio yatasaidia taifa kuondoa mmomonyoko wa maadili.

"Tunaamini kwamba taasisi za dini zina mchango mkubwa katika kulinda maadili ya nchi yetu. Watengenezaji maudhui katika mitamdao ya kijamii na vyombo vya habari, nao wana umuhimu mkubwa, ninavihi watusaidie katika hilo," alisema Dk. Ndumbaro.

Klele cha tamasha hilo ni Septemba 23 mwaka huu, likitarajiwa kufungwa na Rais Samia Suluhu Hassan.

# Naibu Waziri ahimiza usafi mazingira kuvutia watalii

**Na Robert Hokororo**

NAIBU Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Khamis Hamza Khamis amesema usafi wa mazingira ni jukumu la kila mmoja ambalo anapaswa kulitekeleza.

Khamis alitoa kauli hiyo jana wakati akiongoza wananchi wa kufanya usafi katika eneo la Soko la Mavunde, Chang'ombe, jijini Dodoma kuadhimisha Siku ya Usafi Duniani.

Aliwahimiza wananchi kufanya usafi katika makazi yao na maeneo ya biashara, jambo alilosisitiza ni muhimu kwa ustawi wa afya ya binadamu ili kukabiliana na maradhi.

Naibu Waziri Khamis alisema kuwa si vizuri kuacha taka zikazagaa ovyo kwa kuwa huzalisha bakteria na kusababisha changamoto mbalimbali, bila kusahau uzalishaji kemikali hatarishi kwa binadamu na viumbe hai wengine.

Aliwaomba wananchi kuunga mkono maelekezo ya serikali kufanya usafi wa mazingira hususan kila Jumamosi ya mwisho wa mwezi na siku zingine ili kuweka miji katika hali ya usafi.

"Mnakumbuka Rais wetu kila anaposimama kuzungumza na wananchi katika maeneo mbalimbali, anazungumzia usafi wa mazingira, hivyo nasi hatuna budi kumuunga mkono katika jitihada hizo," alisisitiza Naibu Waziri Khamis.

Alisema watalii wanaokuja nchini kuangalia vivutio wanahitaji kukuta hali ya usafi, hivyo kuvutiwa na kutangaza zaidi nchi, hatua itakayohamasisha watalii kuja kwa wingi.

Mratibu wa Kampeni ya Mtu ni Afya kutoka Wizara ya Afya, Anyitike Mwakitalima, alisema Siku ya Usafi Duniani inahusiana moja kwa moja na Wizara ya Afya ambayo ina dhamana ya kudhibiti magonjwa.

Alisema, "kaulimbiu ya maadhimisho hayo isemayo 'Uhai hauna mbadala, zingatia usafi wa mazingira', inadhihirisha kuwa ili tuwe hai tusipate maradhi, lazima watu wazingatie usafi wa mazingira."

Mwakitalima alipongeza Ofisi ya Makamu wa Rais, serikali kwa ujumla na wananchi wa eneo la Chang'ombe kwa kushiriki katika usafi kuzunguka soko hilo, hatua aliyoitaja itaamsha ari kwa wananchi wengine kufanya usafi.

Alitoa wito kwa wananchi kuhakikisha usafi hauishii Siku ya Usafi Duniani, bali uwe endelevu.

Mkurugenzi wa taasisi isiyo ya kiserikali ya GoPlant, Emmanuel Likuda alisema Siku ya Usafi Duniani inatambuliwa na Umoja wa Mataifa na inafanyika katika nchi nyingine duniani.



# Mbunge achukua hatua wananchi kupumzika katika banda hospitalini

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Dodoma Mjini, Anthony Mavunde, ameanza ujenzi wa jengo la kisasa la kupumzikia wananchi wanaouguza wagonjwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma.

Ni baada ya kubaini wanakumbana na adha mbalimbali wanapolala na kuishi kwenye banda la nje ya geti la hospitali hiyo.

Banda hilo limewekwa na uongozi wa hospitali hiyo mahali pa kupumzika watu wanaokwenda kuwaona wagonjwa, wakisubiri muda wa kuingia wodini ufike.

Watu ambao wanatoka mikoani na ambao hawana ndugu jijini Dodoma, wamekuwa wakitumia banda hilo kujihifadhi katika kipindi chote wanapouguza ndugu zao.

Akizungumza jana wakati wa uzinduzi wa ujenzi wa jengo hilo, Mavunde ambaye pia ni Waziri wa Madini, alisema jambo hilo lilimwumiza kwa muda mrefu na kuamua kusaidia ujenzi huo kama sadaka kwa wananchi wa ndani na nje ya Mkoa wa Dodoma.

"Ujenzi huu ni sehemu ya utatuzi wa changamoto zinazowakabili wananchi, hapo nje ya eneo la hospitali kuna jengo ambalo wanakaa wananchi ambao asilimia kubwa hawaishi katika Jiji la Dodoma na wanatumia sehemu ile kama sehemu ya kupumzika kusubiri muda wa kuwaona wagonjwa wao," alisema.

"Kuna baadhi yao ambao hawana sehemu ya kulala na hawana makazi Dodoma na hawawezi kurudi walipotoka kutokana na umbali na gharama za usafiri.

"Kuna wakati mwingine kinamama, kinababa na watoto wanachanganyikana na kulala sehemu moja, kulingana na maadili ya kitanzania si vyema sana kuchanganyika watu wa jinsi tofauti sehemu moja na hasa ambao kwa namna moja au nyingine hawana uhusiano wowote.

**"Ujenzi huu ni sehemu ya utatuzi wa changamoto zinazowakabili wananchi, hapo nje ya eneo la hospitali kuna jengo ambalo wanakaa wananchi ambao asilimia kubwa...**

"Jambo hili lilinigusa sana nikasema moja ya sadaka, Mungu akinijalia na nitapenda niache kama alama ni kuwahifadhi na kuwasitiri wananchi wangu ambao wanakaa katika eneo lile ambalo lipo wazi," alisema.

Mavunde alisema katika jengo hilo litatenganishwa eneo la wanawake na wanaume na huduma zote walizotegemea kuzipata ndani ya hospitali.

"Jengo hili tumeanza ujenzi leo na litajengwa kwenye mfumo nadhifu wasipate adha wakati wa baridi na mvua, nitafunga TV ya kisasa, nitajenga choo na sambamba na hilo nafahamu wanaokaa pale hawamudu vyakula vya hotelini na kuna mamantilie wamekuwa wakiondolewa.

"Ninachoomba jiji lisiwaondoe wale mamalishe na kama kuna namna yoyote ya kuweka mazingira mazuri kulinda afya, mtaniambia nipo tayari kuweka eneo zuri pia kwa ajili yao ili watoe huduma kwa hawa wananchi," alisema.

Kaimu Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo, Dk. Sarah Ludovick alisema hospitali hiyo ina miaka 104 na ilianza kama kituo cha afya na imekua na kufikia hadhi ya kuwa hospitali ya mkoa.

Alisema hospitali inatoa huduma kwa kuzingatia sera, miongozo na taratibu zilizowekwa na Wizara ya Afya na kutumia fursa hiyo kumshukuru Mbunge Mavunde kwa moyo wake wa kutatua changamoto iliyokuwa inawakabili wananchi.

Mwenyekiti wa Dodoma Legends , Ahmad Toufiq ameonesha kufurahishwa na kuanza ujenzi huo na kuahidi wao watachangia mifuko 100 ya saruji kuunga mkono juhudi hizo.



Mtendaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania, Prof. Elisante Ole Gabriel (katikati), akizungumza wakati wa ufunguzi wa semina kuhusu Maboresho na Uongozi wa Kimkakati katika Mnyororo wa Utoaji Haki kwa Baraza la Uongozi la Chama cha Mawakili Tanganyika (TLS), jijini Dodoma mapema wiki hii. Kushoto ni Rais TLS, Wakili Boniface Mwabukusi na Mkurugenzi Mtendaji wa Chama hicho, Mariam Othman. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# 'Wekezeni katika elimu ya watoto wenu kupata viongozi wa baadaye'

**Na Peter Mkwavila,** CHEMBA

MWAKILISHI wa Ubalozi wa Ireland nchini ameshauri wazazi na walezi ilayani Chemba, mkoani Dodoma kuwekeza kwenye elimu ya watoto wao ili wafikie ndoto zao na kupata viongozi wa baadaye.

Suzanne Keatinge alitoa rai hiyo alipozungumza na wakazi wa Kijiji cha Makamaka, wilayani Chemba wakati wa ziara yake ya kutembelea miradi mbalimbali iliyofadhiliwa kwa kushirikiana na mashirika ya Counsenuth, Agha Khan Foundation na TGNP.

Alisema ili waweze kufanikiwa katika kujiletea maendeleo, wanatakiwa kuwekeza kwa watoto wao kielimu kwa kuwasomesha na kuwaendeleza.

"Mtaji wa maendeleo kwa nchi yoyote ni pale unapowapata wasimamizi wenye elimu na taaluma. Ili kufikia malengo hayo, wazazi na walezi ni muhimu mkawekeza kwa watoto wenu kielimu badala ya kuwaacha bila kusomeshwa," alisema.

Mwakilishi huyo pia aliwaomba wananchi hao kuendelea kutoa ushirikiano kwa mashirika na taasisi zinazowekeza miradi ya maendeleo katika maeneo yao ili iwaletee maendeleo kiuchumi.

Aliwaomba taka wananchi hao kuendelea kushirikiana na wawekezaji kufanya kazi kwa pamoja ili kuleta tija kimaendeleo kwa pande zote.

Awali, Mkuu wa Shule ya Msingi ya Makamaka, Yahaya Kimolo, akitoa taarifa ya shule hiyo ambayo ni moja ya zilizopata ufadhili na ubalozi huo kwa kuwekewa matangi ya kuvunia maji kwa ajili ya matumizi mbalimbali, alisema shule hiyo bado inakabiliana na uchakavu wa baadhi ya madarasa.

# TARI yatoa mafunzo kwa wakulima, maofisa ugani

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) Naliendele imeanza kutoa mafunzo kwa wakulima na maofisa ugani wa Halmashauri ya Wilaya ya Singida kuhusu kilimo cha korosho ili kuongeza uzalishaji wa zao hilo litakalowasaidia kujikwamua kiuchumi.

Mafunzo hayo yalianza kutolewa juzi katika shamba la mkulima Mustapha Mwangi lililoko Kata ya Ilongero, lengo likiwa kupunguza athari za wadudu na magonjwa yanayoweza kupunguza uzalishaji na tija ya zao hilo.

Akizungumza wakati wa mafunzo hayo, Mtafiti kutoka TARI, Gaspar Mgimiloko alisema wameanza kutoa mafunzo hayo kwa wakulima ili kutambua umuhimu wa matumizi sahihi na salama ya viwatilifu ili kudhibiti visumbufu vya korosho.

Alisema wakulima hao watafundishwa namna ya upuliziaji viwatilifu, matumizi ya mavazi kinga, mbegu bora, utunzaji shamba, uchanganyaji mazao na upogoleaji.

Mgimiloko alisema mafunzo haya ni muhimu kwa maofisa hao hasa wale waajiriwa wapya, ili kuongeza uelewa wao kuhusu uzalishaji korosho, hususan wanaotoka maeneo ambayo hayana uzoefu na zao hili.

"Lengo la kuwajumuisha wakulima na maofisa ugani, tunaamini maofisa ugani tayari wana mafunzo walioyapata vyuoni, lakini kuna maofisa ugani ambao ni waajiriwa wapya na yamkini wanatoka sehemu au kanda ambazo hazilimi korosho, lengo pia ni kuwaongezea wigo wa uelewa juu ya uzalishaji zao la korosho," alisema.

Mkulima Emiliana Lisu kutoka Kata ya Kinyagigi, aliahidi kuyafanyia kazi mafunzo aliyoyapata ikiwa ni pamoja aina na matumizi sahihi ya viuatilifu, namna nzuri ya upandaji korosho pamoja na ujuzi kuhusu udongo unaofaa.

Mmiliki wa shamba lililotumika kwa mafunzo, Mwangi, alieleza namna mafunzo yalivyomsaidia kufahamu thamani ya kilimo cha korosho na kuboresha shamba lake ambalo awali halikutoa mavuno mazuri.





## Tume ya Ukimwi Z'bar yatengewa bil. 33.4/-

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

JUMLA ya Sh. bilioni 33.4 zimetengwa na Serikali ya Zanzibar kwa ajili ya kuiwezesha Tume ya Ukimwi kuongeza kasi ya mapambano dhidi ya ugonjwa wa Ukimwi pamoja na kufuatilia makundi maalumu ikiwamo vijana kuona yanadhibitiwa.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Harusi Said Suleiman, alisema hayo wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Mwanakwerekwe, Ameir Abdalla Ameir, katika kikao cha Baraza la Wawakilishi Chukwani jana, aliyetaka kujua mikakati ya kupambana na Ukimwi kupitia Tume ya Taifa ya Kudhibiti Ukimwi ikoje.

Suleiman alisema Tume hiyo imepewa majukumu mengi ikiwamo kuhakikisha maambukizi yanayotokana na ugonjwa huo yanapungua kwa kiasi kikubwa.

Aidha, aliitaja mikakati mengine ikiwamo kutoa elimu ya kupambana na Ukimwi kupitia makundi mbalimbali hatarishi ambayo yanaongoza kwa maambukizi mapya.

Akitoa takwimu, alisema maambukizi mapya yamepungua kwa kiasi kikubwa kuanzia mwaka 2005 na ni mwaka ambao serikali ilianzisha huduma za matibabu kwa waathirika wa ugonjwa wa ugonjwa huo ikiwamo kuwapatia dawa kwa watu wanaoishi na VVU.

Alisema kwa miaka minne iliyopita maambukizi ya ugonjwa huo yamepungua kutoka watu 519 waliopata maambukizi mapya kwa mwaka 2020 hadi 362 kwa mwaka 2023.

Alisema kwa mwaka 2024 hadi kufikia Julai ni watu 213 ambao waligundulika na maambukizi mapya ya virusi vya Ukimwi ambao tayari wanatumia dawa za kufubaza maradhi hayo.

"Mheshimiwa Spika takwimu hizo zinaonesha kwamba idadi ya watu wanaopata maambukizi mapya mwaka hadi mwaka inaendelea kupungua ikiwamo wananchi wenyewe kuwa tayari kujitokeza kupima afya zao," alisema.

Aliyapongeza mashirika ya kimataifa yanayopambana na ugonjwa wa Ukimwi kwa misaada yao mikubwa ambayo imesaidia kupunguza kasi ya ugonjwa huo.

# Mwinyi ajivunia ajira za sekta isiyo rasmi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi amesema sekta isiyo rasmi inaendelea kutoa mchango mkubwa katika kuzalisha ajira nchini ili kufikia lengo la kuimarisha uchumi wa nchi.

Alisema hayo jana wakati akifunguwa Tamasha la Pili la "FAHARI YA ZANZIBAR" lilofanyika katika viwanja vya biashara vya Nyamanzi, Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja.

Alisema ni jambo la kutia moyo kuona kuwa serikali tayari imeshajenga masoko katika Mamlaka zote za Serikali za Mitaa Unguja na Pemba pamoja na kuendelea kukamilisha ujenzi wa masoko mengine makubwa katika Mkoa wa Mjini Magharibi, hatua ambayo itaongeza ajira.

Alisema yote hayo lengo lake ni kuwawekea wajasiriamali na wafanyabiashara mazingira mazuri ya kufanyia shughuli zao ili kujikwamua kiuchumi.

"Nimejulishwa pia kwamba hatua za kuwapatia mikopo wafanyabiashara kwa ajili ya kukuza mitaji yao tayari zimeanza kutekelezwa," alisema Dk. Mwinyi.

Alisema serikali anayoongoza imekuja na utaratibu mpya wa kutumia asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa kutoa mikopo kwa makundi maalum (asilimia nne kwa wanawake, asilimia nne vijana na silimia mbili watu wenye ulemavu).

Alisema pamoja na kuchelewa kuanza kwa programu hiyo kutokana na utunishaji wa mfuko huo na kuweka utaratibu mzuri wa kibenki katika kusimamia ukopeshaji fedha hizo, tayari vikundi mbalimbali vimeanza kufaidika na mikopo chini ya programu hiyo ambayo inatolewa kupitia Benki ya TCB.

Dk. Mwinyi alisema lengo kuu la mpango huo ni kuwawezesha wananchi kiuchumi ili wajiajiri na kuzalisha ajira kwa wengine.

Alisema kuwa katika utekelezaji dhamira ya kuimarisha mazingira ya uwezeshaji wananchi kiuchumi, serikali imetekeleza miradi ya maendeleo, ukiwamo ujenzi wa barabara za mijini na vijijini ili kurahisisha usafiri wa watu na bidhaa na kuyafikia masoko kwa urahisi na haraka.

Alisema kutekelezwa kwa miradi hiyo kumechangia kwa kiasi kikubwa kuwavutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi na kukuza sekta ya utalii.

"Sekta ya Utalii ina mchango mkubwa katika kuzalisha ajira hasa kwa vijana pamoja na kutoa soko la uhakika kwa bidhaa zinazozalishwa na wajasiriamali wetu," alisema.

Rais Dk. Mwinyi alisema kuwa katika kipindi kifupi cha kuanzishwa kwa Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Zanzibar (ZEEA), kuna upatikanaji mitaji pamoja na marejesho yake yakiimarika sambamba na utoaji mafunzo kwa wajasiriamali pamoja na juhudi za kuwaunganisha na masoko ya ndani na nje ya nchi.

Alisema kuwa katika programu ya Inuka, serikali iliweka Sh. bilioni 15, lakini kutokana na juhudi za usimamizi na ufuatiliaji wa karibu katika marejesho ya fedha hizo, zimewezesha kutolewa mikopo yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 30.2 ambayo ni zaidi ya mara mbili ya fedha iliyowekwa awali.

"ZEEA imekuwa mstari wa mbele katika kubuni na kutafuta miradi mbali mbali kwa lengo la kuongeza nguvu katika mikakati ya kuwawezesha wananchi kiuchumi.

"Tumefahamishwa hapa kwamba ZEEA inaingia katika utekelezaji mradi wa pamoja wenye thamani ya Sh. bilioni 13 kwa ufadhili wa Benki ya Dunia ambao utatekelezwa kwa ushirikiano na Wizara ya Ustawi wa Jamii, Jinsia Wazee na Watoto," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Air Pay Tanzania ambao ndio wadhamini wa tamasha hilo, Yasim Chali alisema kwa kushirikiana na ZEEA wameazisha mfumo wa kuwawezesha wajasiriamali kupata mkopo kwa njia ya kidigitali.

Alisema hatua hiyo inasaidia kuharakisha upatikanaji mikopo na kuachana na utamaduni wa zamani wa kuomba mkopo kwa kuandika karatasi kisha kupeleka katika taasisi zinazotoa mikopo, zikiwAmo benki.

Mkurugenzi Mtendaji wa ZEEA, Juma Burhan alisema wanaendelea kuwawezesha wananchi kiuchumi kwa kuweka mazingira rafiki ili kufikia lengo la kupunguza umaskini kwa wananchi wa Zanzibar.

Alibainisha kuwa hadi kufikia Agosti 31 mwaka huu, wakala kupitia mfuko wa uwezeshaji, umetoa mikopo yenye thamani ya Sh. bilioni 33.1 kwa wajasiriamali.




Wadau wa maendeleo wa Wilaya ya Rorya, mkoani Mara, akiwamo mbunge wa zamani wa Rorya Lameck Airo (wa tatu kulia), wakiangalia mabati 100 yaliyotolewa na Mjumbe wa Mkutano Mkuu CCM Taifa, Sango Gungu wilayani humo juzi, kwa ajili ya kuezekea madarasa mawili ya Shule ya Sekondari Kirongwe. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali kuendelea kuweka mazingira bora ya sanaa

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Zanzibar kupitia Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, imesema itaendelea kuweka mazingira bora ya kuendeleza sanaa na utamaduni wa Mzanzibari kwa maslahi mapana ya vizazi vya sasa na baadaye.

Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla aliyasema hayo wakati akisoma hotuba kwa niaba ya Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, katika hafla ya ufunguzi wa Tamasha la 29 la Utamaduni wa Mzanzibari lililofanyika uwanja wa Misuka, Mahonda Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Alisema serikali imeanza ujenzi wa nyumba ya Sanaa Mwanakwerekwe kwa lengo la kuviendeleza vipaji vya wasanii na wajasiriamali wanatengeneza bidhaa za utamaduni na itakapomalizika itatumika kwa kufundishia sanaa na vitu vya utamaduni ambavyo vitasaidia kuitangaza Zanzibar nje ya nchi sambamba na kutoa fursa kwa wahitimu kujiajiri wenyewe.

Hemed alisema sekta ya utalii inaendelea kukua kwa kasi kubwa visiwani Zanzibar na kutoa nafasi kwa Wazanzibari kuzitumia bidhaa za kiutamaduni na vyakula vya asili ambavyo vinawavutia watalii wengi wanaongia na kutoka Zanzibar na kuchangia kuongezeka kipato.

Aidha, alitaka Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kuwaandaa walimu wenye sifa na uwezo ambao watakaoutumia kuwafundisha vijana na kutambulika duniani kote pamoja na kuajiriwa katika hoteli, kampuni binafsi na serikalini. Hemed aliwahakikishia wazanzibari kuwa serikali itaendelea kutoa kila aina ya ushirikiano katika kufanikisha maadhimisho ya Tamasha la Utamaduni wa Mzanzibari na matamasha mengine ili kuenzi na kudumisha fikra na falsafa za waasisi wa taifa.

Naye waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Tabia Maulid Mwita, alisema wizara yake kupitia Idara ya Utamaduni na Sanaa, ikitoa elimu ya kulinda utamaduni wa Mzanzibari kupitia vyombo vya habari kwa lengo la kuhakikisha mila, silka na utamaduni wa Mzanzibari unaendelea kulindwa na kudumishwa vizazi na vizazi.

Alisema Wizara ya Habari haitasita kuwachukulia hatua wote watakaobainika kutokulinda na kuvunja utamaduni za Mzanzibari ambao umekuwa ukiitangaza Zanzibar kupitia sanaa mbalimbali.



**RUBBY**
UKURASA 12





# DIAMOND, MAVOKO KUMBE HAWANUNIANI

STAA wa muziki wa bongo fleva nchini, Rich Mavoko amesema hana mawasiliano kwa muda mrefu na Diamond Platnumz kwa sababu siyo washkaji, lakini kama ikitokea wakakutana hawatonuniana, bali watasalimiana.

Mavoko ambaye kwa sasa anatamba na goma lake 'Kill my Self', akimshirikisha Chinno, alisema tangu alipomaliza biashara yake pale WCB hawajawa na mawasiliano, ingawa haiwafanyi kutosalimiana wakikutana.

"Hatujawahi kuwa washkaji , tulikuwa tunafanya biashara ambayo ndiyo ilitukutanisha,imeisha kila mtu anafanya mambo yake, maisha yanaendelea," alisema Mavoko.

Akaongeza kuwa ingawa hana urafiki wa kihivyo na Diamond Platnumz, lakini wakikutana wanasalimiana kama kawaida.

"Tulikutana kazini sisi ni watoto wa kiume, hatuwezi kununiana tunaongea tunasalimiana, hata tukikutana leo, kesho tunasalimiana tunaongea lakini kusema eti ushkaji kinomanoma, hapana ni kama tu wafanyakazi wanavyokutana ofisini," alisema.

## BASI SAWA

### Tundaman atakiona Chamoto



Msanii wa muziki wa bongo fleva, Tundaman, ametoa ngoma yake mpya aliyoipa jina la 'Chamoto', na imeshaanza kunyanyasa kwenye vyombo vya habari.

Tundaman, ambaye ni mmoja wa wasanii wachache wanaopiga muziki wa aina nyingi, ikiwemo bongo fleva, R&B, singeli, mduara na staili zingine aliipua ngoma hiyo siku sita zilizopita kwa mfumo wa audio, ambapo bado yupo kwenye mchakato wa kuitoa kwa mfumo wa video.

"Kumbe upo macho, napiga hujapokea, sasa kifuatacho kuna kitu kitatokea, kama kiendacho kwa mganga hakitarejea. Hela nalipa mimi unanilaza nje, kweli samaki mbichi ndiyo inatakiwa umkunje, kwa usingizi gani haijapita sekunde. Leo cha moto utakiona, kule ushebe mama , leo cha moto utakiona." Inasikika baadhi ya mistari ya ngoma hiyo.

### Billnas kama Dk. Remmy Ongala




Baada ya kupiga onyesho lililofana sana wiki iliyopita, msanii Billnas amesema anatamani kurudi tena Mwanza.

Alisema kwa jinsi walivyopafumu, walivyopokelewa na kushangiliwa, anatamani kufanya tena onyesho katika jiji hilo.

"Yaani ilikuwa balaa, natamani kurudi tena Mwanza." Alisema Billnass. Maneno hayo yalishawahi kusemwa miaka mingi iliyopita na mwanamuziki, Dk. Remmy Ongalla, katika wimbo wake wa Mwanza.

Baada ya kufunya onyesho kubwa, alirejea Dar es Salaam na kutunga wimbo uliokuwa na mashairi kuwa anarejea tena Mwanza kama alivyosema Billnas.



# DIAMOND AONJESHA NGOMA YAKE MPYA

Diamond Platnumz ametoa kiojo cha ngoma yake mpya ambayo haijatoka. Ameshea ngoma hiyo kwenye mtandao wake wa instagram. Akiwa kwenye gari na mtayarishaji wa muziki, S2Kizzy walionekana wakiimba ngoma hiyo.

"Waliona mwaka happy new year, kula pombe mpaka upande juu ya meza, chezea juu, leta misosi kula, maisha yenyewe wanga ni wengi," ni baadhi ya mashairi yaliyokuwa kwenye ngoma hiyo ambayo bado hata jina lake haijulikani na lini itaachia kwa mashabiki.

Baada ya kionjo hiyo, mashabiki wengi wanaonekana kulisubiri kwa hamu pini hilo ambalo linaonekana ni la kuchezesha zaidi.



# Ruby usiseme yote

Msanii Ruby, amefunguka na kuweka kazi kwa mara ya kwanza ni kweli ameacha na mzazi mwenzake, lakini akamtuhumu kuwa amemtapeli.

"Mimi na huyu kama tumeachana sijawahi kuleta mambo yasiyofaa, kulea mtoto shida, sapoti mkono wa dirisha, sikutaka kabisa tuwe maadui, nimekuheshimu sana, lakini naona heshima haikupendezi. Nikuvumilia sana mwisho imetosha, unafikia hata kunitapeli mimi mzazi mwenzako, ama kweli duniani kuna vitu na vituko." Haya ni baadhi ya maneno ambayo yamemtoa mwanadada huyo kwenda kwa mzazi mwenzake.

Wazee wa zamani walisema mkiachana msiseme yote na wala msimalize maneno, huwezi jua, ipo siku mnaweza kurudiana, kwa sababu dunia ni duara.

## FILAMU

# Sauna, mke wa kurithi

**Na Adam Fungamwango**

KUNA mila za Kiafrika ambazo bado zipo zinaendelea kufuatiliwa na ni nzuri kwa sababu zinautambulisha utu na heshima yake, lakini zipo zilizopitwa na wakati.

Hapa leo tutaiangalia filamu ya 'Sauna', ambayo inamhusu jamaa mmoja aliyepewa mke wa marehemu kaka yake, lakini kilichokuja kutokea ni msukosuko kwenye familia yake.

Wakati mwingine hao wanapewa wake za marehemu wanakuwa na wachumba zao ambao wameahidiana kuona, hivyo kunakuwa na mvutano, kisasi na mambo mengine yanayofanana na hayo.

Imechezwa na wasanii wengi sana, kina Walykister Michael, Salum Nambende, Rikia Mkalomba, Aloyce Joseph, Cauthly Amir na wengineo wengi.

Nambende na mpenzi wake Zakia ambaye waliahidiana kuwa wataonana. Hata hivyo mipango si matumizi.

Kaka yake anafariki, hivyo ndugu na wazee wanataka amrithi mkewe. Pamoja na Nambende kukataa, lakini anaambiwa mila ndivyo ilivyo, hivyo hakuna atakachoweza kubadili.

Kabla ya kutekeleza hilo anakwenda kumwambia mpenzi wake Zakia. Inakuwa ni huzuni kubwa kwa mpenzi wake, kwani analia na kuona ndoto zote walizopanga zimepotea.

Nambende anamrithi mke wa kaka yake na katika ndoa yao, wanabahatika kupata mtoto aitwaye Sauna.

Sauna anakuwa msichana, lakini Zakia bado alikuwa na lake rohoni. Bado alimpenda Nambende na alikuwa hajakata tamaa ya kutaka kuolewa naye.

Anakwenda kwa mganga na kupewa vitu ambavyo vingeweza kumsaidia kuifanya ndoa ya Nambende na mkewe isambaratike.

Pamoja na kwamba Nambende ameoa, lakini mapenzi yao yanaonekana kuwa yalikuwa yanaendelea kama kawaida.

Kuna siku walikutana sehemu na Zakia akamweleza mpenzi wake kuwa mkewe na binti yake ni wachawi.

Nambende akaonekana kupinga kitu hicho, lakini mpenzi wake anampa uthibitisho na kumwambia aende kwa mganga ili akathibitishe hilo.

Nambende na rafiki yake wanakwenda huko, na wanaambiwa kama Zakia alivyosema. Kumbe Zakia tayari ameshaongea na mganga kuhusu kitu hicho.

Kilichotokea ni kwamba wanapewa dawa ili wakampe mtu fulani. Wanapofika njiani wanakutana na mtu huyo. Wanampa dawa ambayo wamepewa na mganga. Hata hivyo walivyompa tu, mtu huyo aligeuka kuwa Sauna.

Baada ya hapo Sauna hakuwa tena kama mtu wa kawaida, bali kama nusu binadamu na nusu mzimu.



# MAPRODUZYA WALIOTISHA BONGO FLEVA

**Na Adam Fungamwango**

KWA sasa muziki wa bongo fleva hapa nchini umekuwa ukitamba kimataifa. Tanzania ni moja kati ya nchi ambazo muziki wa kizazi kipya umekuwa ukipendwa na kuheshimiwa sana nje ya mipaka yake.

Wasanii mbalimbali kwa sasa wamekuwa maarufu na wanapiga pesa ndefu kutokana na ngoma zao mbalimbali.

Mwanzo haikuwa rahisi. Muziki wa kizazi kipya ulionekana kuwa ni wa kihuni wakati unaanza kutanua mbawa zake mwishoni mwa miaka ya 1990 na mwanzoni mwa miaka ya 2000.

Kuna watu wanapaswa kupewa heshima zao kwa kuondoa kuonekana kuwa ni wa kubuni na kufanya wa heshima kupendwa na hata watu wazima.

Joseph Mbilinyi maarufu kama Sugu na Joseph Haule, Profesa Jay ni moja kati ya wasanii wachache walioigeuza bongo fleva kutoka ilikotoka na kuwa hapa leo ilipo.

Hiyo ni kwa upande wa uimbaji, lakini pia wapo watu nyuma yao, wanaitwa maproduzya. Hawa ni watayarishaji wa muziki.

Ndiyo wanaowatafutia wasanii hao mirindimo kwenye nyimbo zao wanazotambia.

Wakati wa kupigania mapinduzi ya bongo fleva kukiwa na nyimbo za hip hop, R&B, zouk miaka hiyo, wapo maproduzya ambao nao walikuwa na mchango mkubwa kwenye kuifanya tasnia hiyo kukubalika.

**Mika Mwamba**

Jina lake kamili ni Miikka Aleksanteri Kari raia na Finland. Wasanii na mashabiki wa muziki wanamtabua kama Mika Mwamba.

Anatajwa kuwa ndiye mtayarishaji muziki bora zaidi kwenye muziki wa kizazi kipya. Umaarufu wake ulikuwa mkubwa kuanzia miaka ya 2000, alipofatengenezea ngoma kali wasaa kama Dully Sykes, Inspector Haroun, Lady Jay Dee, Mad Ice, Chegge, Mandojo na Domo Kaya, Solid Ground Family, Complex, Zahrani (maarufu kama Big Punisher wa Bongo), Only Face, Dknob, Daz Nundaz na wengineo.

**P Funk**

Huyu ni mtayarishaji muziki na mmiliki wa Studio ya Bongo Records. Jina lake kamili ni Paul Matthysse. Ni mmoja wa maproduzya waliowapandisha chati wasanii wengi kama Solo Thang, AY, Zay B, Sista P, Mike T, Ze Pungu, Jay Mo, Chege, Temba, na baadhi ya wasanii wa TMK, pia alishawahi kufanya kazi na Profesa Jay, Afande Sele, Ferouz. Wengine ni Mr Il Sugu, Monduli Mobb, Gangwe Mobb, Hop Pot Family ikiongozwa na Soggy Doggy, na Manyema Family.

**Master J**

Anaitwa Joachim Kimario, maarufu kama Master J. Ni mtayarishaji aliyewekeza kwenye studio kadhaa tofauti, na moja ya sifa zake ni kwamba mbali na bongo fleva, lakini pia mtayarishaji wa muziki wa kwaya, pamoja na muziki wa dansi pia. Bendi nyingi za dansi kipindi hicho kama FM Academia, African Stars 'Twanga Pepeta', TOT Plus zilikuwa zikienda kurekodi kwenye studio zake, chini yake mwenyewe. Moja ya studio zake maarufu ni MJ Production.

**Henrico**

Ni mmoja wa watayarishaji maarufu wa muziki wa bongo fleva ambaye naye huwezi kumuacha kwenye orodha ya watayarishaji walioibeba tasnia ya muziki wa kizazi kipya, akifanya kazi na wasanii wengi nchini.

Henrico alikuwa kinara studio ya Soundcrafters.

**Said Comorien**

Wasanii wa zamani wa bongo fleva na mashabiki wake hawawezi kumsahau Said Comorien. Alikuwa mtayarishaji muziki alifanya kazi na wasanii mbalimbali, akiwemo Rehema Chalamila, maarufu mama Ray C na wengineo.

Metro Studio, ndiyo alikuwa akiimiliki.



# Oxlade kumbe mwoga

MWANAMUZIKI wa Nigeria Oxlade, amesema aliacha masomo yake ya chuo kikuu na kutoroka nyumbani kutokana na vitisho kutoka vikundi vya wahuni.

Akizungumza hivi karibuni, Oxlade katika chuo yeye alikuwa mvulana mtanashati na kusababisha magenge ya wahuni kumlenga na kutaka kujiunga nao,

"Niliacha chuo kikuu katika mwaka wangu wa mwisho kwa sababu ulikuwa wakati mgumu kwangu. Kulikuwa na magenge ambayo walitaka nijiunge nao, kuwa mvulana mzuri hukufanya kuwa shabaha. Ni ama ujiunge nao au wanakuacha ukiwa taabani. Kwa hivyo ilibidi niache mazingira hayo,"



## Shaggy hana furaha tena

MWIGIZAJI na mchekeshaji kutoka Nigeria, Broda Shaggi amefichua kuwa ameponea chupuchuku kukatisha maisha yake katika tukio la kutisha.

Shaggi alitumia ukurasa wake wa Instagram kuandika ujumbe mzito katika siku yake ya kuzaliwa ambao alisema kwamba usiku wa kuamkia siku hiyo alipata tukio hilo la kutisha na kusababisha kukata tamaa.

"Lakini siku hii ya kuzaliwa ni tofauti kwa sababu zawadi ya uhai ilikaribia kuchukuliwa kutoka kwangu hivi majuzi lakini Mungu alijidhihirisha na kunipa nafasi nyingine." ameandika bila kutaja tukio hilo.


## IK awajia juu wachungaji feki

MSANII wa filamu wa Nollywood IK Ogbonna, amesema anakerwa na wachungaji feki kutokana na vitendo vyao vinavyokejeli Ukristo.

Kupitia chapisho lake kwenye Instagram, Ogbonna amesema wachungaji wanaojihusisha na vitendo vya ulaghai vya kutoa miujiza bandia inadhihaki dini hiyo yenye waumini wengi nchini humo.

"Matendo haya yanatia doa kiini cha kweli cha Ukristo, yakigeuza imani kuwa tamasha kwa ajili ya kujinufaisha ubinafsi. Matokeo yake? Uaminifu uliovunjwa unapoteza maisha, na imani inabadilishwa kwa faida," amesema.





## P Diddy katengwa mahabusu

HATIMAYE rapa mkongwe kutoka Marekani, Sean Combs, maarufu kama Diddy, amepandishwa kizimbani na kusomewa mashtaka ya kuendesha biashara ya ngono na ulaghai.

Waendesha mashtaka waliiambia mahakama kuwa rapa huyo alifanya biashara hiyo kuanzia 2008, ambayo ilichanganyika na dawa za kulevya na kuwafanyia unyanyasaji wanawake ka kuwalazimisha kufanya ngono.

Kulingana na CNN, Combs atakuwa mahabusu ya peke yake katika kitengo maalum cha kizuizi cha Metropolitan jijini New York, hadi kesi yake itakapoanza kusikilizwa.

## Portable kalizua tena

MWANAMUZIKI mwenye utata, Portable, ameibua gumzo baada ya kukumvamia mchungaji ambaye alikwenda kuhubiri mbele ya baa yake.

Katika klipu iliyosambaa mtandaoni, Portable alionekana akimpiga kofi mchungaji huyo aliyekuwa akihubiri karibu na baa ya mwimbaji huyo katika mji wa Sango Ota jimbo la Ogun.

Kitendo hicho kilikosolewa na watu mbalimbali hasa kutoka kwa waumini wa dini ya Kikristo ambao walieleza sawa na kufanya shambulio katika mwili wa Yesu.







Mkuu wa Polisi kikosi cha usalama barabara Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, Mkaguzi Msaidizi wa Polisi, Wilfred Natale (kulia), akitoa elimu ya usalama barabarani kwa madereva wa pikipiki na bajaji wanaobeba abiria wa mji mdogo wa Mirerani, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Laini za simu milioni 35 zaunganishwa intaneti

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WAZIRI wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Jerry Silaa amesema laini za simu za mkononi zaidi ya milioni 75 zinatumiwa na Watanzania kwa ajili ya mawasiliano, huku laini milioni 35 zikiunganishwa moja kwa moja na huduma ya mtandao wa intaneti.

Waziri Silaa alibainisha hayo jana jijini Arusha wakati akifungua Kongamano la Connect 2 Connect lililowakutanisha wadau wa sekta ya mawasiliano wa ndani na nje ya nchi.

Alisema kuwa kupitia kongamano hilo, watajadiliana kuunganishwa kidigiti kusiwe tu kupata Intaneti, bali kuwapo uhakika wa huduma yenye kasi, isiyokuwa na hitilafu na kwa gharama nafuu kwa watumiaji.

"Tumewakutanisha wadau kujadiliana kuhusu mafanikio tuliyoyapata kwa kuwaunganisha wananchi na itaneti, pia kuangalia njia za kufikia muunganiko bora zaidi ya huu tuliokuwanao sasa ili kuchochea shughuli za kiuchumi na kijamii," alisema Waziri Silaa.

Waziri huyo alisema kuwa kutokana na kazi iliyofanywa na serikali, wamefanikiwa kufikisha huduma za mawasiliano ya intaneti kwenye maeneo mbalimbali nchini kwa mfumo wa 3G kwa asilimia 89, 4G kwa asilimia 83 na 5G kwa asilimia 15.

Alisema kwa hali ya dunia hivi sasa intaneti imebeba maisha ya watu kwa kuwa shughuli nyingi, zikiwamo za kilimo na biashara zinafanyika huko.

Alisema kwa maeneo ambayo hayajafikiwa na mawasiliano, serikali imejipanga kuhakikisha minara ya mawasiliano inasimikwa ili kurahisisha upatikanaji huduma hiyo kwa wananchi.

"Serikali Mei 2023 ilizindua mkakati wa ujenzi wa minara 758 kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) ili tupeleke huduma kwenye maeneo ambayo hayana," alisema.

Waziri Silaa alisema mbali na minara 758, kuna minara mingine 636 inajengwa na mradi utaanza Oktoba mwaka huu kuhakikisha maeneo yote nchi yanapata mtandao wa simu, intaneti, redio na televisheni.

Kuhusu hali ya usalama wa kimtandano, waziri huyo alisema Tanzania iko vizuri kwa kuwa ni moja ya nchi zilizowekeza vizuri kwa kuwa kuna kitengo cha kudhibiti uharamia wa mawasiliano ndani ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kinachosimamia masuala ya kimtandao na kuratibu masuala ya usalama wa kimtandao katika kila sekta.

"Serikali itahakikisha Watanzania wanafanya shughuli zao za kiuchumi na kijamii kupitia kwenye mitandao wanakuwa salama kwa kuwa tuna mifumo imara ya kimtandao," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Helios Towers, Gwakisa Stadi, alisema kampuni hiyo nchini inasimamia minara zaidi ya 400 na wana wateja zaidi ya 10,000 ambao ni watumiaji wa minara hiyo.

Alisema kazi kubwa ya mirana hiyo ni kuunganisha huduma za mawasiliano na wateja wao wakubwa ni kampuni za mawasiliano ya simu, kampuni za usambazaji intaneti na televisheni zilizoweka vifaa vyao vya mawasiliano kwenye minara hiyo.

"Kazi yetu kubwa tunaunganisha, kujenga na kusimamia minara na tumedhamini kongamano hili, kwa kuwa maono ya kampuni yetu ni kuwaunganisha Watanzania na mataifa mengine ya Bara la Afrika na nchi za Mashariki ya Kati," alisema mkurugenzi huyo.

# Maofisa Ustawi wa Jamii wabaini tatizo katika nyimbo, mavazi ya wasanii nchini

**Na Mary Mosha,** MOSHI

MWENYEKITI wa Maofisa Ustawi wa Jamii nchini, Martin Chuwa, ameshauri serikali kufuatilia nyimbo za wasanii nchini na mavazi yao na kuweka msimamo wa aina za nyimbo zinazopaswa kupigwa nchini.

Alitoa rai hiyo juzi wakati wa ufunguzi wa mkutano wa mwaka wa maafisa ustawi wa jamii uliofanyika katika Shule ya Polisi Tanzania, mkoani Kilimanjaro.

"Iko haya ya serikali kuangalia upya nyimbo pamoja na wasanii wetu, hali yao ya mavazi na kuweka msimamo rasmi wa nyimbo hizo kutopigwa kwenye maeneo, kama magari, TV, redio na badala yake ziwe zinapigwa maeneo ya kumbi za starehe tu ili kuepusha kuendelea kuharibu jamii," alisema.

Chuwa pia alisema maofisa ustawi wa jamii wanakabiliwa na changamoto ya bajeti kidogo inayokwamisha utendaji kazi wao.

Naibu Waziri wa Fedha, Hamad Hassan Chande, alisema kuna haja Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kuelekeza kila ofisi ya maofisa ustawi wa jamii inayojengwa kuanzia sasa, iwe na miundombinu rafiki.

Pia alimwagiza Naibu Katibu Mkuu - TAMISEMI anayeshughulikia miundombinu, Rogatus Mativila, kuhakikisha wanatenga vyumba vya ofisi za ustawi wa jamii vyenye miundombinu rafiki katika halmsahuri nchini ambavyo vitazingatia faragha za wateja wanaowahudumia.

Naibu Waziri alisema kuwa hivi sasa maofsa hao wanafanya kazi kwenye vyumba visivyo na staha wala faragha, jambo ambalo wakati mwingine wateja hao kushindwa kujieleza na kupata msaada uliotarajiwa.

"Ninyi TAMISEMI mnasimamia haya mambo, hakikisheni kila halmashauri kunakuwa na eneo la kutosha lenye faragha ya kutosha kusikiliza wateja wao, ili iwasaidie kutoa huduma katika mazingira mazuri na yatakayoweza kuleta matokeo chanya kwa jamii tunazozihudumia kwa kuzingatia ramani inayotolewa na wizara," alisema.

Chande alisema maofisa hao wanafanya kazi katika mazingira magumu na kutaka TAMISEMI kuangalia namna ya kusaidia kwa haraka utatuzi wa changamoto hiyo.

Naibu Waziri Chande pia aliwataka wazazi na walezi kushirikiana na maofisa ustawi wa jamii katika malezi na makuzi ya watoto ili kuondoa tatizo la ukatili kwa watoto.

"Katibu Mkuu TAMISEMI hakikisha unatoa maelekezo kwa makatibu tawala wa mikoa nchini kuelekeza halmshauri kutunga sheria ndogo za kuwawajibisha wazazi au walezi ambao hawatoi malezi kwa watoto wao," aliagiza.

Alisema kuwa matukio ya ukatili kwa watoto yanaongezeka ambapo asilimia 60 ya matukio hutokea katika ngazi za familia huku asilimia 40 ya matukio yakitokea ndani na nje ya shule, hali inayorudisha nyuma Maendeleo.

Awali, Naibu Waziri wa Maendeleoya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mwanaidi Ally Hamis, alielekeza halmashauri zote kutenga asilimia tatu ya mapato kwa ajili ya maofisa ustawi wa jamii ili waweze kutoa huduma kwa ufanisi.

"Kazi wanayofanya maofisa hawa ni ngumu, na wateja wao ni sisi sote, tunatofautiana nyakati, hivyo tuweke mazingira salama na kutenga bajeti ili iweze kusaidia katika kufikia jamii," alisema

## Mbunge apongeza halmashauri kubana matumizi kujenga uwanja

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

MBUNGE wa Babati Mjini, Pauline Gekul, amesema mradi wa ujenzi wa uwanja wa kisasa wa mikutano na michezo uliotekelezwa Kwaraa, umetokana na halmashauri hiyo kubana matumizi.

Amesema uwanja huo uliobatizwa jina la 'Tanzanite Kwaraa', wakati wa ujenzi wake, kuna wakati walibana matumizi hata kusababisha miradi ya maendeleo kusimama ili wafanikisha mradi huo.

Gekul alisema hayo jana wakati akikabidhi jezi na mipira kwa kata zote nane za halmashauri hiyo ili kuruhusu kuanza michuano ya Samia Cup na Gekul Cup katika Jimbo la Babati Mjini.

"Kuna wakati tulisimamisha miradi mingine ili uwanja huu ujengwe, tulipambana madiwani mpaka ukajengwa na sasa umeanza kutumika ila tunaendelea na ujenzi," alisema Gekul.

Aliongeza kuwa katika ligi hiyo atakayoanzisha, zaidi ya tim 86 zitachuana kwa lengo la kuibua vipaji vya vijana ili wanufaike na kuanza kwa michuano ya ligi kuu kupitia uwanja wa kisasa uliojengwa Babati.

Mbunge huyo alisema wanatamani michezo hiyo ifanyike kila mtaa na kila kijiji ili washiriki hata watoto wadogo na vipaji vyao viibuliwe.

Gekul alisema kuwa kupitia kujengwa kwa uwanja huo wa kisasa na ligi kuu kuutumia, Halmashauri ya Mji wa Babati itaanza kupata asilimia 15 ya mapato kutoka kila mechi ya Ligi Kuu itakayochezwa.

Vilevile, alieleza kuwa mashindano hayo yatatumika kuhamasisha wananchi kushiriki Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na kujiandikisha kwenye Daftari la Wakaazi.

Mmoja wa viongozi wa Chama cha Mpira wa Miguu la Wilaya ya Babati, Gerald Mtui, alisema michezo ni ajira, ndio maana wameamua kuibua vipaji vya vijana kuanzia ngazi za vijiji na mitaa.

Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Babati Mjini, Cholaje Cholaje, alisema vikiibuliwa vipaji vya vijana vitasaidia kupunguzia mzigo serikali wa kutafuta ajira.

Cholaje alisema michezo hiyo itatumika kuhamasisha Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na aliahidi kuendelea kusimamia serikali ili itenge maeneo ya wazi kwa ajili ya michezo.

MAKALA

## TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA...

# Miaka 45 ya kifo cha Tindwa beki kitasa wa Simba aliyefia uwanjani

-Alianguka ghafla mechi ikiendelea, hakuinuka tena

-Ndiye mchezaji pekee wa Simba aliyekufa akiipigania nembo



Kikosi cha Simba cha Katikati ya miaka ya 1970.

**Na Adam Fungamwango**

ILIKUWA ni Jumamosi, Mei 12, 1979, hali ya hewa ya jiji la Dar es Salaam haikuwa na jua na joto kama ilivyo kawaida.

Jua lilimezwa na mawingu kwa muda mwingi siku hiyo, huku kukiwa na manyunyu ya mvua. Siku hiyo kulikuwa na mechi ya mkondo wa kwanza, raundi ya pili ya Klabu Bingwa Afrika, ambalo kwa sasa linaitwa Ligi ya Mabingwa Afrika.

Wakati huo lilichezwa kwa mtoano kuanzia mwanzo mpaka mwisho anapopatikana bingwa.

Mechi iliyokuwa ichezwe siku hiyo ilikuwa ni kati ya Simba dhidi ya Racca Rovers kutoka Nigeria.

Tangu enzi na enzi, mashabiki wa Simba wakishaona hali hiyo ya hewa na wakati wana mechi basi furaha moyoni, wimbo mdomoni kwani wanajua watashinda mchezo huo.

Simba ilikuwa imeingia hatua hiyo baada ya kufanya maajabu kwa kuiondoa kwenye michuano hiyo, Mufulira Wanderers ya Zambia kwa jumla ya mabao 5-4. Ni baada ya kufungwa mabao 4-0 Uwanja wa Taifa, Dar es salaam (sasa Uhuru), na kwenda kuisambua timu hiyo nyumbani kwao, mabao 5-0 katika mchezo wa marudiano.

Wakati mchezo unaendelea, beki wa kati, Hussein Tindwa aliruka juu na mchezaji mmoja wa Racca Rovers, kuupiga kichwa mpira wa krosi kuondoka hatari langoni mwake, mara baada ya kucheza mpira huo, alidondoka chini na hakuinuka tena.

Mwamuzi wa mchezo, alipuliza filimbi kusimamisha mchezo ili kumwangalia alikuwa amepatwa na masahibu gani, alimkuta mchezaji huyo amepoteza fahamu, inadaiwa damu zilikuwa zikimtoka masikioni, puani na mdomoni.

### ALIFIA UWANJANI

Mchezaji wa kwanza wa Simba kufika eneo la tukio, alikuwa ni Mohamed Kajole (naye sasa ni marehemu) ambaye wakati tukio hilo linatokea alikuwa karibu yake kwa sababu wote ni mabeki katika fikra zake, Kajole alidhani Tindwa alikuwa amepoteza fahamu tu.

Tukio hilo lilitokea katika dakika za mwisho kabla ya mapumziko. Tindwa alitolewa uwanjani kwa kubebwa na machela na baada ya kuonekana tatizo lake lilikuwa kubwa, aliingizwa kwenye gari la wagonjwa kupelekwa hospitali. Ukweli ni kwamba tayari alikuwa ameshafariki dunia pale pale uwanjani.

Lakini pia kuna wengine waliodai kuwa alifia njiani kabla ya kufikishwa kwenye Hospitali ya Taifa Muhimbili, wengine wakidai baada ya kufikishwa.

Ukweli alifariki akiwa uwanjani, na wachezaji wa Simba wakafichwa taarifa hiyo kwani bado walikuwa na kibarua cha dakika 45 zingine, kipindi cha pili. Mchezo huo uliisha kwa suluhu. Na baada ya mchezo kumalizika ndipo kifo chake kikatangazwa.

### KILITIKISA NCHI

Kusema kweli kifo chake kilitikisa nchi, wanamichezo wengi walipatwa na simanzi, ambapo klabu mbalimbali pamoja na Chama cha Soka Nchini wakati huo kikiitwa (FAT), vilisikitishwa, vikatoa salamu za rambirambi na michango mbalimbali ilitolewa ambapo Baraza la Michezo la Taifa limetoa shilingi 2,000, FAT shilingi 1,500, Wafanyakazi wa Wizara ya Utamaduni na Vijana shilingi 685, klabu ya Chui Shilingi 300, Coastal Union ya Tanga, Yanga na Chama cha Kandanda mkoani Dar es Salaam shilingi 500, kila moja na Wafanyakazi wa Bandari walichanga shilingi 131 wakati huo zilikuwa pesa nyingi sana.

### MAZISHI YAKE

Mazishi yake yalifanyika siku tatu baada ya kifo chake, Jumanne, Mei 15, 1979, ambapo, Waziri wa Utamaduni wa Taifa na Vijana Chadiel Mgonja, aliongoza maelfu ya waombolezaji na wanamichezo kumzika mchezaji huyo.

Balozi wa Nigeria nchini Tanzania, Kamisaa wa pambano kati ya Simba na Raccah Rovers, Tambwe Mgandelu kutoka Zaire (sasa DRC) na viongozi wa vyama mbalimbali vya michezo, walionekana kujawa na huzuni wakati maiti ya marehemu ilipokuwa mazishini.

Wachezaji wote wa Simba walifika kwenye mazishi hayo na walilia waziwazi wakati maiti ya marehemu ikiteremshwa kaburini, wakiwa na majonzi makubwa ya kumpoteza rafiki na mchezaji mwenzao.

Kekeke za vilio vilisikika kuanzia nyumbani kwa akina mama na kila jeneza lilipopita, hadi makaburini, na kila sehemu hali ilikuwa ya majonzi makuu.

Alizikwa kwenye makaburi ya Mwinyimkuu, Magomeni Mapipa, jijini Dar es Salaam.

Mbali na Waziri Mgonja, waliopatoa hotuba zao siku hiyo mazishini ni Mwenyekiti wa Simba Luka Luhui.

Mwenyekiti wa FAT, Said El Maamry, Mwakilishi wa Balozi wa Nigeria, kiongozi wa Racca Rovers, na Katibu Mkuu wa Yanga Christopha Mahimbo.

### UGONJWA WA MOYO

Kifo cha mchezaji huyo kilizua maneno mengi, kila mtu alikuwa akizungumza lake.Beki huyo wa kati, ndiyo kwanza alikuwa ameanza kuaminiwa, akiwa bado kinda, akisajiliwa kutoka Majimaji ya Songea na kupoteza maisha uwanjani kwa kiasi kikubwa lilihusishwa na imani za ushirikina.

Wapo waliodai mganga wa Simba alimkabidhi hirizi Tindwa kwa niaba ya timu kwa ajili ya kuweza kusaka ushindi katika mchezo huo na kuna wanaoamini mambo hayo wanasema, mganga wa Simba alizidiwa na ndumba za Racca Rovers na kusababisha kifo cha Tindwa.

Hata hivyo, ripoti ya madaktari walioufanyia uchunguzi mwili wa marehemu ikabainisha kuwa marehemu Tindwa alifariki kutokana na maradhi ya moyo.

### MAISHA YAKE

Alizaliwa jijini Dar es Salaam na kuzichezea klabu za Tambaza, baadaye Breweries, kabla ya kwenda Majimaji ya Songea. Jina lake halisi ni Hassan Tindwa, lakini Simba walimbadilisha jina na kumwita Hussein ili kutofautisha yule wa Majimaji na Simba kwani angefungiwa kwa kusaini timu mbili.

Hii ya kubadilisha majina kwa mchezaji yule yule ilitumika sana na klabu mbalimbali miaka ya nyuma ili kukwepa adhabu hiyo na anachofanya ni kubadili jina la timu ambalo anataka kuichezea kuwa ndiyo la kwake halisi.

Imetimia miaka 45 sasa baada ya kifo hicho kilichotikisa, ingawa klabu ya Simba haifanyi kumbukumbu, na mashabiki wake hawaelimishwi, wala hawakumbushwi kuhusu kuwepo kwa mchezaji huyo, ili kumuenzi mchezaji huyo pekee wa klabu hiyo, aliyefia uwanjani akiipigania nembo ya klabu hiyo.

HABARI KIMATAIFA

# Rwanda yaanza kutoa chanjo ya mpox

**KIGALI,** RWANDA

RWANDA imeanza kampeni ya kutoa chanjo dhidi ya ugonjwa wa mpox kwa kutumia dozi 1,000 iliyopokea kutoka Nigeria chini ya makubaliano kati ya nchi hizo mbili.

Hayo yalibainishwa jana na kituo cha kuzuia na kudhibiti magonjwa barani Afrika, Afrika CDC.

Daktari Nicaise Ndembi kutoka kituo cha Afrika CDC alisema kuwa zoezi hilo la kutoa chanjo lilianza siku ya Jumanne na lililenga wilaya saba zenye watu walio katika hatari kubwa wanaoishi kwenye mipaka jirani ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Nigeria ilitoa dozi 1,000 kwa Rwanda kutoka kwenye mgao wa dozi 10,000 ambazo ilipokea kutoka Marekani.

Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo imekuwa kitovu cha mlipuko wa ugonjwa wa mpox barani Afrika ambako wagonjwa wapya 2,912 na vifo 14 vimeripotiwa katika muda wa wiki moja iliyopita, na kupelekea idadi jumla ya wagonjwa wa mpox kuwa 6,105 na vifo 738 tangu mwanzoni mwa mwaka huu.

"Lazima tuzuie mlipuko wa ugonjwa wa mpox haraka sana," alisema mkurugenzi mkuu wa kituo cha kuzuia na kudhibiti magonjwa barani Afrika, Afrika CDC Daktari Jean Kaseya.

Kasema alieleza kuwa Rwanda na nchi nyingine zimetoa wito wa kutolewa kwa dozi zaidi tofauti na ya walizozihitaji awali.

Wataalamu wa afya barani Afrika wamekadiria kuwa bara hilo litahitaji takriban chanjo milioni 10 ili kuzuia mlipuko wa mpox.

Ilielezwa kuwa serikali ya Japan imesaini makubaliano na serikali ya Kongo kutoa dozi milioni 3 za chanjo dhidi ya mpox.

Mkurugenzi mkuu wa shirika la afya duniani (WHO) Tedros Ghebreyesus alizihimiza nchi zaidi kuchangia katika kukabiliana na kusambaa kwa mpox.

"Ushirikiano wa kimataifa na msaada unahitajika ili kuzuia kuenea kwa virusi vinavyosababisha ugonjwa wa mpox," Ghebreyesus aliandika kwenye mtandao wa kijamii wa X zamani ukijulikana kama Twitter.

Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo inatarajiwa kuanza kampeni ya kutoa chanjo katika wiki ya kwanza ya mwezi Oktoba.

Ilibainishwa kuwa takriban dozi 165,000 zimewasili nchini humo, huku nchi kadhaa za Ulaya zikiahidi kutoa chanjo zaidi kwenda Kongo.

"Tunahitaji chanjo dhidi ya mpox ianze kutengenezwa barani Afrika, na tunafanya kazi kwa karibu na kampuni za kutengeneza chanjo na washirika wetu ili chanjo zitengenezwe katika moja ya nchi za Afrika," Kaseya alisema.

WHO siku ya Ijumaa imeidhinisha kwa mara ya kwanza matumizi ya chanjo dhidi ya mpox kwa watu wazima, ikieleza kuwa ni hatua muhimu katika kupambana na ugonjwa huo barani Afrika.

Kuidhinishwa kwa chanjo iliyotengenezwa na kampuni ya Bavarian Nordic A/S kunamaanisha wafadhili kama vile Gavi na UNICEF wanaweza kuinunua chanjo hiyo.

Hata hivyo, ilielezwa kuwa usambazaji bado ni mdogo kwa sababu ni kampuni moja tu ndio inayotengeneza chanjo hiyo.

**DW**



Muuguzi nchini Rwanda akimchoma chanjo mwananchi. **PICHA: MTANDAO**

# Pande hasimu Sudan ziko tayari kutafuta suluhu

**KHARTOUM,** SUDAN

KIONGOZI wa kijeshi wa Sudan pamoja na hasimu wake kamanda wa vikosi vya msaada wa haraka (RSF), kwa pamoja wamesema wako tayari kutafuta suluhu ya vita inayoendelea nchini humo kwa miezi 17 hivi sasa.

Msingi wa kauli na msimamo huo ulitokana na kujibu wito wa Rais wa Marekani Joe Biden, alioutoa siku chache zilizopita.

Hata hivyo, majenerali hao wawili wameendelea kulaumiana kwa kushindwa kumaliza mapigano na ukiukaji wa haki za binadamu dhidi ya raia, bila yao kuweka bayana, mikakati ya kufikia mwafaka kwa njia ya amani.

Wapatanishi katika mazungumzo yaliyoratibiwa na Marekani jijini Geneva, waliripoti makubaliano ya kuimarisha upatikanaji wa msaada wa binadamu, japo upande wa jeshi ambao haukuwakilishwa katika mazungumzo hayo, ulitajwa kuwa kikwazo.

Ilielezwa kuwa watu zaidi ya 12,000 wamewauwa katika mapigano hayo ambayo pia yamesababishwa watu zaidi ya milioni 10 kuwa wakimbizi.

**RFI**

# India yakanusha kuipa Ukraine silaha

**NEW DELH,** INDIA

INDIA imepuuzilia mbali ripoti ya habari inayodai kuwa serikali ilishindwa kuwazuia wanunuzi wa Ulaya kuhamisha makombora yaliyotengenezwa na India hadi Ukraine.

Katika taarifa iliyochapishwa Alhamisi, Reuters ilidai kwamba makombora yaliyouzwa na watengenezaji silaha wa India kwa wateja wake wa Ulaya yalielekezwa kwenda Ukraine.

Ripoti hiyo ilidai kuwa uhamishaji wa silaha umekuwa ukiendelea kwa zaidi ya mwaka mmoja, huku Delhi ikiwa haichukui hatua yoyote kukomesha hilo licha ya maandamano ya mara kwa mara kutoka Moscow.

Wizara ya mambo ya nje ya India imeita ripoti hiyo kuwa ni uvumi na ya kupotosha.

Ripoti hiyo inamaanisha ukiukaji wa India, ambako hakuna kitu kama hicho kilichotekelezwa, na kwa hivyo, sio sahihi na ni yenye nia mbaya," Randhir Jaiswal, msemaji wa wizara hiyo aliandika kwenye mtandao wa X (zamani ulijulikana kama Twitter).

Jaiswal aliongeza kuwa India ina rekodi inayoweza kufuatiliwa kikamilifu na majukumu yake kimataifa juu ya kutoengeza silaha na ina sheria zake dhabiti za usafirishaji. Ilielezwa kuwa Moscow bado haijajibu ripoti hiyo au taarifa ya Delhi. Huku Ukraine, ambayo inapambana na mashambulizi mapya kutoka kwa Russia, inaripotiwa kukabiliwa na uhaba wa risasi na silaha zingine.

**BBC**

# Polisi yazuia mkutano wa Lissu

**Na Waandishi Wetu**

JESHI la Polisi mkoani Tanga limezuia mkutano wa hadhara wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) uliopangwa kuhudhuriwa na Makamu Mwenyekiti wake, Tundu Lissu kwa madai kuwa una dalili kubwa za kuleta uvunjifu amani.

Kutokana na zuio hilo, Mwenyekiti wa CHADEMA, Wilaya ya Tanga, Rashid Jumbe, alisema jana kuwa Jeshi la Polisi halikutenda haki kwa kuzuia mkutano huo ambao ulitakiwa kufanyika jana kwa kigezo kwamba viongozi wao walisema watafanya maandamano.

Zuio hilo lilitolewa juzi kupitia barua iliyotolewa na Mkuu wa Polisi Wilaya ya Tanga, D. Mwambigiri, huku nakala ikielekezwa kwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Mkuu wa Wilaya ya Tanga na Mkuu wa Usalama Wilaya ya Tanga.

Barua hiyo yenye kumbukumbu namba GB.774/795/01/71 iliyotolewa kwenda Ofisi za CHADEMA Wilaya, imerejea barua ya chama hicho kiliyoliandikia Jeshi la Polisi yenye kumbukumbu 25/MH/CDM/9/24 ya Septemba 18 mwaka huu kuhusu mkutano wa hadhara utakaohudhuriwa na Lissu.

Taarifa ya polisi ilieleza kuwa imepiga marufuku mkutano huo kutokana na sababu za kiusalama.

"Ikumbukwe kwamba viongozi wa CHADEMA taifa wametangaza nia ovu ya kufanya maandamano siku Septemba 23 mwaka huu, jijini Dar es Salaam.

"Kutokana na taarifa tulizonazo ni kwamba, mkutano wa hadhara unaotakiwa kufanyika kesho (jana Septemba 20) ni maandalizi ya kufanya maandamano mara baada ya kumaliza mkutano huo.

"Kwa mujibu wa mamlaka niliyonayo kutokana na K/f 44 cha Sheria ya Jeshi la Polisi na Polisi Wasaidizi Sura 322, ninazuia kuwapo mkutano huo, kwani una dalili kubwa za kuleta uvunjifu wa amani ndani ya wilaya na kuhatarisha usalama wa rai ana mali zao," ilielezwa katika taarifa hiyo ya Jeshi la Polisi.

Kutokana na hilo, Jeshi la Polisi limesema kukiukwa kwa maelekezo hayo ni kosa la jinai kwa mujibu wa K/f 45 cha Sheria cha Jeshi la Polisi na Polisi Wasaidizi na kwamba, watashughulikiwa kwa mujibu wa kanuni ya adhabu Sura 16, marejeo ya mwaka 2022.

**KAULI YA CHADEMA**

Jumbe alisema lengo lao halikuwa maandamano bali mkutano pamoja na kwenda kutoa pole kwa kada wa CHADEMA, marehemu Ally Kibao nyumbani kwake maeneo ya Makorora, jijini Tanga.

"Sisi kama CHADEMA Wilaya ya Tanga tumelaani kitendo hiki na hii inaonesha kwamba, serikali yetu haijatenda haki kwa jambo hili," alisema.



Meneja Masoko wa Taasisi ya Karimjee Foundation, Cobus Zyl (katikati), akiwakabidhi tuzo ya ushindi wa jumla wanafunzi wa Shule ya Sekondari Lumumba ya mjini Zanzibar, Salha Khamis (kulia) na Ramlat Abdulla, wakati wa hafla ya kukabidhi tuzo za wanasayansi vijana chipukizi yaliyoandaliwa na Taasisi ya Wanasayansi Chipukizi Tanzania (YST), jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mwigulu ahimiza matumizi nishati safi ya kupikia Afrika

**Na Benny Mwaipaja**

WAZIRI wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba ametoa wito kwa nchi za Afrika kutafuta njia na mikakati ya kuboresha uchumi na maisha ya wananchi wake kwa kutumia nishati safi ya kupikia.

Amesema hatua hiyo pia itasaidia kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi yanayochangiwa na uharibifu wa mazingira.

Dk. Nchemba alitoa wito huo mjini Antananarivo, Madagascar juzi kwa niaba ya Rais Samia Suluhu Hassan wakati akihutubia katika Mkutano wa Mwaka wa Wanahisa wa Taasisi ya Africa50 (General Shareholders Meeting - GSM) na Jukwaa la Miundombinu la Afrika (Infra for Africa Forum meeting). Tanzania ni mwanachama wa Taasisi ya Africa50

Waziri Nchemba alishauri nchi hizo kuwekeza katika kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa wananchi wao kutumia nishati safi ya kupikia pamoja na faida zinazoambatana na utunzaji mazingira kiuchumi na kijamii.

Dk. Nchemba pia alitoa wito kwa taasisi za fedha na sekta binafsi kushiriki katika kampeni ya matumizi ya nishati safi ya kupikia, ikiwamo gesi iliyosindikwa, nishati ya jua na umeme wa joto ardhi kwa kuwezesha upatikanaji fedha na pia kuzalisha vifaa ama majiko yanayotumia nishati hiyo.

Katika msafara huo, Dk. Nchemba aliambatana na Naibu Katibu Mkuu anayesimamia Fedha za Umma, Amina Khamis Shaaban na Balozi wa Tanzania Madagascar, Mwenye makazi Maputo, Msumbiji, Faustine Kasike.

Mkutano wa Wanahisa wa Africa50 unatarajiwa kuwakutanisha wadau mbalimbali kutoka Bara la Afrika na duniani kwa ujumla wakiwamo wawekezaji kutoka taasisi za umma na sekta binafsi, wakopeshaji, wataalamu wa ujenzi wa miundombinu na kuwawezesha kutafuta suluhisho la changamoto za miundombinu katika Bara la Afrika pamoja na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

## Watatu wapandishwa kizimbani shtaka kuwaua mama, mwanawe

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WATU watatu wamefikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Dodoma na kusomewa mashtaka ya kuua mama na mwanawe mkoani Dodoma.

Akisoma hati ya mashtaka mbele ya Hakimu Mkazi wa mahakama hiyo, Dennis Mpelembwa, Wakili wa Serikali Mwandamizi Patricia Mkina alidai washtakiwa hao wakabiliwa na kosa la kuwaua Salma Ramadhani (11) pamoja na mama yake mzazi, Mwamvita Mwakibasi (33).

Katika kesi hiyo ya mauaji namba 26982 ya mwaka 2024, Wakili Mkina aliwataja washtakiwa hao kuwa pamoja na ni Fikiri Senyagwa (35), maarufu Baba Chichi, mkazi wa Ipagala, jijini Dodoma.

Wengine ni Daudi Nyakongo (34), mkazi wa Mkonze jijini na Rajabu Rashidi (45), mkazi wa Mkonze jijini. Wote kwa pamoja wanashtakiwa kwa kosa la kuwaua watu hao wawili.

Wakili Mkina alidai kuwa tukio hilo lilitokea Septemba 6 mwaka huu katika Kata ya Mkonze, jijini Dodoma ambapo watu hao wanadaiwa kuvamia na kuwafanyia vitendo vya ukatili kisha kuwaua mama na mwanawe.

Kesi hiyo imeahirishwa hadi Oktoba 4 mwaka huu itakapotajwa mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi Zabibu Mpangule wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Dodoma.

Iwapo watathibitika kutenda mauaji hayo, adhabu yake ni kifungo cha maisha kwa mujibu wa Sheria ya Kanuni, Sura 16.

**Wengine ni Daudi Nyakongo (34), mkazi wa Mkonze jijini na Rajabu Rashidi (45), mkazi wa Mkonze jijini. Wote kwa pamoja wanashtakiwa kwa kosa la kuwaua watu hao wawili.**

# HADITHI

TAARIFA ya Jeshi la Polisi inatangaza kuokotwa na maiti ya msichana mzuri na mrembo mno Mariamu, maeneo ya Tabata pembezoni mwa barabara mapema alfajiri. Alikuwa amevalia mavazi ya michezo. Alionekana alikuwa anakimbia, ametoka au anakwenda jogging. Taarifa ya madaktari inasema alikufa kwa mshtuko wa moyo, hiyo inaonyesha kuwa alianguka wakati anafanya zoezi alfajiri ile. Ndugu wa marehemu walikataa ripoti, kwani inaonekana kama alipigwa na kitu kizito kilichonasibishwa na chuma kichwani, kilichosabisha kuwa na tundu kichwani. Ndugu wanaliomba Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi wa kina ili kugundua ukweli na wanaapa kuwa kama halikufanyika hilo, damu ya ndugu yao haitoenda bure. Kwani kuna nini? Kila nakala yako ya gazeti la Nipashe, itakupeleka kwenye ukweli wa jambo hili.

# Damu ya Mariamu-31

**Na Adam Fungamwango (0716 350534)**

Baada ya kuridhika usiku wa kwanza alifanya majaribio na kupita kwenye jengo la ofisi hizo.

Afande Willy alimwambia anachotakiwa kukifanya ni kuingia ndani ya jengo hilo, ghorofa ya pili, chumba namba 12, ambamo ndimo zilimo ofisi za Materu. Afande huyo alisema kutokana na intelejensia yake inaonesha kuwa ndani humo, kuna droo ambayo ina siri zote za mazungumzo pamoja na baadhi ya picha za video za mauaji ya Mariamu.

Hivyo akamwambia anatakiwa kuingia humo kwa hila. Na hawezi kuingia kabla ya kukabiliana na walinzi wanaolinda hapo ambao wana silaha nzito. Kuingia kwa kuvamia ndani ya ofisi ya Materu haiwezekani kiusalama kwani wanafanya kazi ambayo Jeshi la Polisi haiitambui.

Kwa maana hiyo wanatengeneza mpango na Kamal kujifanya mwendawazimu anayepita hapo mara kwa mara ili kuwapumbaza walinzi wasiwe naye makini kabla ya kuwavamia. Kamal alipewa bastola na daktari Shija kaka yake afande Willy, kwani afande huyo hakutaka kutoa ya kwake. Lakini Willy akamsisitizia kuwa aitumie pale tu itakapolazimika na aamini sana nguvu zake za mwili.

Masizi aliyojipaka, vumbi, kiroba cha makopo aliyobeba, na nguo chakavu alizovaa, zilimfanya aonekana mwendawazimu. Alionekana ni mwenzawazimu ambaye ndiyo kwanza uamuanza. Bado hajakuwa mchafu zaidi. Bado hajaanza kukimbiza na kupiga watu. Alionekana mpole, asiye machachari, mkali na makeke mengi.

Akaanza kujipitapitisha na kwenda mbali zaidi ya jesho hilo. Kwa muda wa wiki moja alikuwa anapita hapo kwa saa tofauti kiasi cha kuanza kuzoeleka na walinzi.

“Wewe si unatabia za kuchukua wake za watu. Unamuona mwenzake huyo. Wamemtegeneza. We angalia bado kijana tu huyu, lakini keshaharibikiwa.” Mlinzi mmoja alimwambia mwenzake baada ya kumuona akipita maeneo hayo na haikuwa mara ya kwanza. Kamal mwenyewe alisikia maongezi hayo. Akatabasamu kimoyomoyo. Alijua tayari somo lilikuwa limewaingia. “We unaona hilo tu, inawezekana kapata uchizi kwa sababu ya kula ‘ndumu’, ujue bangi nayo inaweza kumfanya mtu akawa mwendawazimu, siyo mke wa mtu tu.” Akajibu mwingine na kusababisha mwenzake aangue kicheko. “Unakwepa eee, maana una tabia hiyo, sasa namwambia iwe bangi, au kuchukua wake za watu, vyote hivyo unaweza ukapata uwendawazimu.”




**Yote hayo hayakuwafanya waache walichokikusudia. Walibebwa na dhamira. Waliona wanachofanya si uhalifu bali ni kutafuta haki. Kuusaka ukweli uliofichwa na watu wabaya kwa makusudi ili watu wema wateseke.**

Wiki iliyofuata akaanza kukaa karibu na jengo hilo lililopo maeneo ya Makumbusho.

Haikuwa tatizo kwao kwani walionekana kama kumzoea na hakuwa mwendawazimu mgomvi. Ingekuwa mtu mwenye akili timamu kwa kazi yao ya ulinzi wasingeweza kumuweka ndani ya mita 100 kutoka kwenye jengo wanalolinda, lakini mtu ambaye hana akili, hawakuwaza hata siku moja mtu mwenye taahira ya akili anaweza kufanya chochote, au kuwazuia wasiendelee na kazi yao, ya kuiba kitu chochote.

Kabla hakujakucha, Kamal kuondoka kwenda eneo ambalo anavua nguo zake za uendawazimu na kurejea nyumbani kwa afande Willy ambako amehamia.

******************************

Siku ya kazi ambayo wenyewe waliamua kuifanya baada ya kujidhihirisha kuwa mambo yote yamekwenda kama yalivyopangwa, walifanya kitu kama mazoezi hivi ili kutofanya makosa.

Katika kazi yake ya upolisi, afande Willy alifanikiwa kupata funguo tatu za bandia ambazo zingefungua mlango mkuu wa jesho hilo, mlango namba 15 ambao ni ofisi ya Materu na ufunguo mmoja wenye uwezo wa kufungua droo zote zilizomo ndani ya ofisi hizo.

Ulikuwa usiku mtulivu. Ilionekana ingepita kama siku zingine. Kamal na afande Willy walikuwa wakiwasiliana kwa meseji tu.

Awali, kama kawaida, alivaa nguo zake za kiwendawazimu. Akawaza kuwa siku hiyo ndiyo ilikuwa anazivaa kwa mara ya mwisho. Lakini hakujua kuwa yote hayo waliyoyafanya yatazaa matunda au vipi. Ulikuwa ni usiku muhimu, na mzito kwao. Kama wakifanikiwa, basi kazi yote ambayo walikuwa wanaifanya itakuwa imefika asilimia 90, na itabaki 10 tu ili kukamilika.

Kujulikana kwa muuaji halisi ya Mariamu na wanachi waamini yote yatatokana na ufanisi wa kazi ambayo wanakwenda kuifanya. Kama haitofanikiwa, mawili, wapoteze maisha wote wawili, mmoja, au hata kama wasipopoteza, wataishia kifungoni kwa kujaribu kuvunja na kuingia kwenye jengo hilo. Si hivyo tu, Kamal atakuwa amejiingiza mwenyewe kwenye mdomo wa mamba, kwani alikuwa anatafutwa kwa kesi ya kumuua mpenzi wake, Mariamu, huku afande Willy akipoteza kazi ya uaskari kwa kosa la wizi na kushirikiana na muuaji.

Yote hayo hayakuwafanya waache walichokikusudia. Walibebwa na dhamira. Waliona wanachofanya si uhalifu bali ni kutafuta haki. Kuusaka ukweli uliofichwa na watu wabaya kwa makusudi ili watu wema wateseke.

Alifika maeneo yale saa nne usiku na kutembea kama kawaida yake. Awawapita walinzi na kwenda kukaa eneo ambalo huwa anakaa. Lakini siku hiyo alikaa mbali kidogo ili kupoteza lengo. Wakati huo alikuwa akimtumia meseji afande Willy aanze kusogea eneo la tukio. Walikuwa wamepaki gari lao nje ya kituo cha mabasi Makumbusho. Afande aliliacha gari na kuanza kusogea taratibu, akilizunguka jengo la kituo cha mabasi ambalo pembeni yake kulikuwa na wauza chips, kuku, sambusa, na vitafunwa vingine.

Saa nane usiku ndiyo muda ambao walipanga kazi ianze kwani mji ulikuwa umetulia sana na hakukuwa tena na pilikapilika za watu. Kamal alipokea meseji kutoka kwa afande Willy kuwa aanze kazi na yeye yupo jirani kuja kumsaidia.

Akiwa na nguo zake zile zile na kuonekana kama mwendawazimu. Alisogea kwa kunyata. Kwake ilikuwa rahisi zaidi kuliko alivyodhani kwani tayari walinzi wake wawili walikuwa wameanza kusinzia. Hakuna yoyote aliyefikiri kuwa kuna hatari inaweza kutokea muda ule. Alinyata kama mwanajeshi vitani. Alifika nyuma ya mlinzi mmoja aliyekaa kwenye kiti. Pigo moja la ngumu lililotua kichogoni lilimfanya mlinzi kuzirai bila kujua nini kimetokea. Wakati mwingine akishtuka kwa kishindo kilichotokea, kamal alirusha teke lililomkata kwenye taya na kusababisha apepesuke. Huyu alikuwa amesimama mbali kidogo na mwenzake. Alipogeuka ndipo alipokutana na kipigo hicho. Wakati akihamanika na kutaka kuweka silaha yake vizuri ili aitumie, alijikuta akipigwa kabali ya nguvu iliyomfanya asalimu amri na kwenda chini taratibu. Alikuwa afande Willy ndiye aliyefanya kazi ile baada ya kuwasili na kukuta tayari mwenzake ameshaanza kazi.

**Itaendelea Jumamosi**

# FEI TOTO ATAKA UBINGWA AZAM

Na Shufaa Lyimo

MCHEZAJI wa timu ya Azam FC, Feisal Salum 'Fei Toto' amesema malengo yake ni kupambana kwa nguvu zote kuhakikisha anaipa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania timu yake msimu huu kwa kucheza kwa kujituma kwenye kila mchezo.

Akizungumza jijini Dar es Salaam mara baada ya kumalizika kwa mchezo wao dhidi ya KMC ambao walishinda mabao 4-0, alisema licha ya kuwepo na ushindani wa namba ndani ya kikosi hicho anaamini hakuna linaloshindikana.

"Ushindani wa namba kwenye timu yetu ni mkubwa isipokuwa nitajituma ili niweze kuipa mafanikio timu yangu," alisema Fei Toto.

Aidha alisema amefurahi kupata tuzo ya kuwa mchezaji bora katika mchezo huo na hiyo ilitokana na ushirikiano aliopewa na wachezaji wenzake uwanjani.

"Ninawashukuru wachezaji wenzangu kutokana na ushirikiano walionipa tulipokuwa uwanjani hadi nikafanikiwa kupata tuzo hii," alisema.

Aliongeza siri ya mafanikio yake imetokana na nidhamu aliyonayo pamoja na kufuata vizuri maelekezo anayopewa na benchi lake la ufundi nje na ndani ya uwanja.

Na aliweka wazi kuwa msimu huu una ushindani mkubwa kwani kila timu imejipanga vizuri.

# Mwasapili aibukia Mbuni FC

Na Adam Fungamwango

BEKI wa zamani wa klabu za Mbeya City na Azam FC, Hassan Mwasapili, amejiunga na klabu ya Mbuni FC kwa ajili ya kuichezea timu hiyo kwenye Ligi ya Championship, ambayo imefanya usajili mkubwa kwa lengo la kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

Mwasapili amejiunga na timu hiyo, baada ya wachezaji wengine wawili waliowahi kuichezea Ligi Kuu kwa mafanikio, golikipa Manyika Peter na Miraji Athumani 'Sheva' waliowahi kuichezea Simba kusajiliwa na timu hiyo.

Taarifa iliyotolewa na klabu hiyo ya maafande yenye maskani yake Arusha, imesema imefanya usajili ambao inaamini utafanikisha azma yao ya kupanda Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

Mwasapili anayecheza beki wa kushoto, ni mmoja wa wachezaji walioipandisha Mbeya City na kucheza Ligi Kuu kwa mafanikio makubwa msimu wa 2013/14.

Mbali na wachezaji hao, klabu hiyo imetangaza wachezaji wengine iliyowasajili ambao ni, Ayoub Laizer, kutoka TMA, Julius John, Danford Kasiwa aliyewahi kuzichezea klabu za Kagera Sugar na Mashujaa, Nasri Daud kutoka Pan African, Mahmoud Juma akisajiliwa kutoka JKU, Juvemtus Fabian kutoka Fountain Gate, Bestie Eliud akitokea Gwambina FC, Khalfan Mohamed kutoka Geita Gold, na Ally Shomari, aliyewahi kuzichezea klabu za Kagera Sugar, Mtibwa Sugar na Simba.



Bendi ya Jeshi la Polisi ikitumbuiza wakati wa hafla ya Maadhimisho ya Siku ya uchunguzi wa Kisayansi Duniani, katika Chuo cha Taaluma ya Polisi Dar es Salaam, Kurasini jana. **PICHA:JUMANNE JUMA**

# Kikapu ya Vijana kutimua vumbi Desemba

Na Shufaa Lyimo

MASHINDANO ya mchezo wa mpira wa kikapu kwa Vijana (JMK Open Tournament) yanatarajiwa kufanyika Desemba 11 hadi 14 mwaka huu kwenye viwanja vya JMK vilivyopo jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe jana, Mratibu wa program za vijana katika kituo cha JMK, Bahati Mgunda alisema mashindano hayo yatashirikisha vijana wenye umri kuanzia miaka 14 hadi 18.

"Mashindano hayo yatashirikisha wasichana na wavulana kutoka mikoa mbalimbali ya Tanzania Bara pamoja na Zanzibar huku baadhi wakitoka nje ya nchi," alisema Mgunda.

Aliitaja baadhi ya mikoa itakayoshiriki kuwa ni Kigoma, Mwanza, Arusha, Singida, Tanga, Unguja na kwa upande wa nje ya nchi ni Kenya na Malawi.

Alisema kwa sasa mchezo huo unazidi kushika kasi tofauti na miaka iliyopita kwa vijana wengi kuonesha nia ya kujifunza mchezo huu.

"Kwa sasa mchezo huu unazidi kukua tofauti na miaka iliyopita kwa vijana kwani, wengi wanajifunza mchezo huu jambo ambalo linatupa matumaini ya kuona Tanzania inaendelea kujiimarisha kwenye michezo," aliongeza kusema Mratibu huyo.

Aidha aliwataka vijana kuwa na mazoea ya kufanya mazoezi mara kwa mara kwa kuwa yanaimarisha afya zao pamoja na kuwasaidia kupata ajira.

# Simba Queens, Yanga Princess kuvaana Oktoba 2

Na Adam Fungamwango

MECHI ya dabi ya soka kwa upande wa wanawake, Simba Queens na Yanga Princess iliyokuwa ichezwe Jumanne ijayo kwenye Uwanja wa KMC Complex, Mwenge, Dar es Salaam, imesogezwa mbele hadi Oktoba 2.

Taarifa iliyotolewa na Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), imesema mchezo huo wa Ngao ya Jamii, sasa utapigwa Oktoba 2 kwenye uwanja huo huo wa KMC.

Hata hivyo, Idara ya Habari na Mawasiliano ya TFF, haikuweka sababu ya kuahirishwa kwa mchezo huo, na mwingine ambao ulikuwa kati ya JKT Queens dhidi ya Ceasiaa Queens uliokuwa uchezwe Septemba 24 saa 7:00 mchana, kabla ya mechi ya watani wa jadi, Simba Queens na Yanga Princess.

Ratiba ya mechi hizo imebaki kama ilivyo, badala yake kilichobadilika ni tarehe ambapo sasa Oktoba 2 kutakuwa na michezo miwili, JKT Queens ikianza saa 7:00 mchana dhidi ya Ceasiaa Queens na saa 10:00 jioni ndipo utakapokuja mtanange huo.

Timu hizo nne zitacheza michezo hiyo ya mtoani ya Ngao ya Jamii, kuashiria kuanza kwa Ligi Kuu ya Wanawake msimu huu.

Ratiba inaonyesha kuwa washindi katika michezo hiyo miwili watacheza fainali ya Ngao ya Jamii itakayopigwa, Oktoba 5, Uwanja wa KMC Complex, Mwenge, Dar es Salaam saa 10:00 jioni, na kabla ya hapo timu ambazo zitapoteza katika michezo hiyo, zitacheza mechi ya kusaka mshindi wa tatu.

Timu zote mbili kwa sasa zipo kwenye maandalizi makali, Mabingwa wa Tanzania Bara, Simba Queens baada ya kuondoka wka Juma Mgunda, ipo chini ya Mussa Hassan Mgosi, huku Yanga Princess ikiamua kumrejesha kocha wake wa zamani, Edna Lema kwa ajili ya kurejesha heshima ya klabu hiyo.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**GORETZKA ATAKIWA MAN UNITED**
KLABU ya Manchester United inaweza kumnunua kiungo wa kati wa Bayern Munich, Leon Goretzka mwenye umri wa miaka 29, huku mustakabali wa kiungo wa kati wa Denmark, Christian Eriksen mwenye miaka 32 na Mbrazil Casemiro mwenye miaka 32, ukiwa bado shakani. (*Manchester Evening News*)

**MAINOO MKATABA MPYA**
MANCHESTER United inatazamia kumpa mkataba mpya kiungo wa kati wa England Kobbie Mainoo mwenye umri wa miaka 19 ili kuonesha hadhi yake kama nyota wa kikosi cha kwanza. (*Fabrizio Romano via YouTube*)

**GYOKERES AGOMBEWA**
KLABU za Tottenham Hotspur, Chelsea na Paris St-Germain zinaongoza katika kinyang'anyiro cha kumsajili mshambuliaji wa Sweden, Viktor Gyokeres mwenye umri wa miaka 26, kutoka kwa wababe wa Ureno Sporting. (*Caught Offside*)

**BREMER KUMRITHI DIJK**
LIVERPOOL inamfikiria beki wa kati wa Juventus na Brazil, Gleison Bremer mwenye umri wa miaka 27, kama mbadala wao bora wa Mholanzi Virgil van Dijk mwenye umri wa miaka 33. (*Teamtalk*)

**EGELI AFUATILIWA MAN**
KLABU ya Newcastle United inamfuatilia mshambuliaji wa Norway, Sindre Walle Egeli mwenye umri wa miaka 18, anayeitwa 'Erling Haaland ajaye', huku West Ham, Crystal Palace, Brighton na Brentford pia zikimtaka mchezaji huyo anayekadiriwa kuwa na thamani ya pauni milioni 25. (*Daily Mail*)

**FRIMPONG ATAKIWA CHELSEA**
MLINZI wa pembeni wa Bayer Leverkusen, Jeremie Frimpong mwenye umri wa miaka 23, yuko kwenye orodha ya wachezaji watano walioteuliwa na Chelsea kuchukua nafasi ya beki wa pembeni wa England, Reece James mwenye umri wa miaka 24. (*TBR Football*)

**WILLIAN ATAJWA PIA**
Chelsea haitamtoa kwa mkopo winga wa Brazil, Estevao Willian mwenye umri wa miaka 17 atakapojiunga na klabu hiyo kutoka Palmeiras msimu ujao wa joto. (*Mail*)

**TOMIYASU AWANIWA INTER**
INTER Milan inataka kumsajili beki wa Arsenal na Japan, Takehiro Tomiyasu Januari huku Washikabunduki wakitaka pauni milioni 25 kwa mlinzi huyo mwenye umri wa miaka 25. (*Daily Mirror*)

**EDERSON MKATABA MPYA**
MANCHESTER City ina nia ya kuanza mazungumzo ya mkataba mpya na golikipa, Ederson mwenye umri wa miaka 31, huku mkataba wa Mbrazil huyo ukitarajiwa kukamilika msimu wa joto 2026. (*TBR Football*)

**JOELINTON KUMALIZIA SOKA BRAZIL**
KIUNGO wa kati wa Newcastle United, Joelinton mwenye umri wa miaka 28, anataka kumalizia soka yake katika nchi yake ya asili ya Brazil. (*Mail*)

**DIBLING KWENYE RADA ZA MAN**
FOWADI wa Southampton mwenye umri wa miaka 18, Tyler Dibling yuko kwenye rada za Manchester United baada ya kumvutia mkurugenzi wao wa michezo, Dan Ashworth. (*Sport*)

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# STERLING AWEKA REKODI YAKE UEFA

**LONDON,** England

### ●●● Awa Mwingereza wa kwanza kuchezea timu nne tofauti za England katika...

WINGA wa Arsenal, Raheem Sterling ameweka rekodi ya kuwa Mwingereza wa kwanza kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na timu nne tofauti za Ligi Kuu England.

Sterling sasa amezichezea timu za Arsenal, Manchester City, Liverpool na Chelsea kwenye michuano hiyo.

Sterling mwenye miaka 29 alijiunga Arsenal akitokea Chelsea mwanzoni mwa msimu huu aliweka rekodi hiyo katika mchezo wa klabu yake hiyo mpya dhidi ya Atalanta kwenye Ligi ya mabingwa Ulaya juzi, alipochukua nafasi ya Bukayo Saka dakika ya 73.

Winga huyo alicheza mchezo wake wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Ulaya Septemba 17, 2014 akiwa kule Anfield wakati Liverpool ikiichapa Ludogorets Razgrad mabao 2-1.

Kisha kucheza tena akiwa na kikosi cha Man City Septemba 15, 2015 ambapo walipoteza 2-1 mbele ya Juventus.

**Akiwa Chelsea Sterling alicheza mchezo wake wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Ulaya Septemba 6, 2022 dhidi ya Dinamo Zagreb, Chelsea ikichapwa 1-0 ugenini.**

Hata hivyo, hakuna timu kati ya hizo zilizotwaa ubingwa wa Ligi hiyo Sterling akiwa sehemu ya kikosi katika msimu wake wa kwanza.

Akiwa Liverpool msimu wa 2014-2015 Liverpool waliondolewa katika hatua ya makundi.

Msimu uliofuata (2015-2016) akiwa Man City klabu hiyo iliondoshwa na Real Madrid kwenye nusu fainali.

Baada ya kuhamia London msimu jana akiwa na Chelsea, klabu hiyo iliishia hatua ya robo fainali kwa kufurushwa na Real Madrid.

Msimu huu yupo Arsenal na tayari amecheza mchezo wake wa kwanza na Arsenal wamepata sare ya bila kufungana.



# ALEXANDER-ARNOLD: NINA FURAHA LIVERPOOL

**LIVERPOOL,** England

TRENT Alexander-Arnold „anafuraha" kuendelea kucheza Liverpool, licha ya tetesi zinazomhusisha na kuhamia Real Madrid.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa England alizivutia timu kadhaa za Ulaya kipindi cha majira ya joto baada ya kujumuishwa katika kikosi cha Gareth Southgate kilichoshiriki Euro 2024.

Mabingwa watetezi wa LaLiga Madrid wamekuwa mstari wa mbele kwa kiungo Alexander-Arnold huku beki huyo wa kulia akikaribia mwisho wa mkataba wake msimu ujao wa joto.

Hata hivyo, sasa inaonekana kama mhitimu huyo wa akademi ya Liverpool anaweza kubaki Anfield kwa muda mrefu, baada ya kushiriki furaha yake kuhusu mustakabali wake na Wekundu hao.

"Kwangu mimi, ilikuwa furaha tu kufanya kazi chini ya kocha mpya ambayo sijawahi kuwa nayo hapo awali," alisema baada ya kikosi chake kupata ushindi wa ufunguzi wa Ligi ya mabingwa Ulaya dhidi ya AC Milan.

"Baada ya kuzungumza na kocha, nilifurahishwa na mipango na jinsi wanavyozungumza kuhusu."

Beki huyo pia alichukua muda kutathmini mwanzo wa maisha ya kikosi chake kwenye Ligi Kuu England na ushiriki wao katika Ligi ya Mabingwa msimu huu.

"Nadhani klabu hii ni ya Ligi ya Mabingwa Ulaya ikiwa na historia ambayo imekuwa nayo na ilisikitisha mwaka jana kutokuwa sehemu yake," aliiambia CBS Sports.

"Lakini tumerudi tunapostahili na hakuna njia bora zaidi ya kuanza kampeni hii kuliko kupata ushindi San Siro.

"Kuna mabadiliko mengi ya kimbinu ndani ya michezo: wapi pa kwenda, wapi usiende, wakati wa kukaa nje, wakati wa kushuka kwenye safu ya nyuma, wakati wa kwenda katikati ya uwanja, wakati wa kuwa kama namba nane, au wakati Mo Salah anaingia ndani na mimi ni winga wa juu."

Alexander-Arnold ameichezea Liverpool mechi tano hadi sasa msimu huu, akisajili asisti moja - katika ushindi wao dhidi ya Milan. Wekundu hao watarejea uwanjani leo Jumamosi watakapowakaribisha Bournemouth kwenye Ligi Kuu England.

# Odobert aipa pigo Spurs

**LONDON,** England

KOCHA wa Tottenham Hotspur, Ange Postecoglou amekiri kuwa ni pigo kubwa baada ya kuumia kwa winga Wilson Odobert.

Spurs walifikia makubaliano yenye thamani ya pauni milioni 30 kumsajili Odobert mwenye umri wa miaka 19 kutoka Burnley wakati wa majira ya joto, lakini alikubwa na jereha la misuli katika mechi yake ya tatu kuanza kwa klabu hiyo na kumfanya atoke nje ya uwanja dakika 18 tu baada ya mechi ya Jumatano ya ushindi wa 2-1 dhidi ya Coventry City.

Alipoulizwa kuhusu hali ya Odobert baada ya mchezo, Postecoglou alikiri: „Ni vigumu kusema.

"Wilson anaonekana ameumia, hivyo tutasubiri tu na kuona."

Odobert hakuwa majeruhi pekee katika mchezo huo kwani Spurs pia ilimpoteza winga mwenzake Timo Werner kutokana na jeraha mwishoni mwa kipindi cha pili.

"Timo, tena sina uhakika kama ilikuwa ni uchovu tu," alisema Postecoglou baada ya kipenga cha mwisho.

"Kwa bahati mbaya wote wawili, wanacheza katika nafasi sawa."



# Eriksen alitakiwa Anderlecht

**MANCHESTER,** England

KIUNGO wa kati wa Manchester United, Christian Eriksen amethibitishwa kuwa alikuwa analengwa na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Anderlecht ya Ubelgiji.

Eriksen alicheza jukumu muhimu katika msimu wake wa kwanza huko Old Trafford, lakini alikua hana nafasimsimu wa 2023/24 kufuatia kuibuka kwa Kobbie Mainoo.

Manuel Ugarte sasa amewasili pia, lakini Mdenmark huyo alifunga mara mbili katika mechi ya hivi majuzi ya Kombe la Carabao dhidi ya Barnsley.

Alihusishwa na kuondoka, ikiwa ni pamoja na kuripotiwa kutakiwa na Real Betis, ingawa klabu hiyo ya Hispania iliachana nae na kumsajili Giovani Lo Celso kutoka Tottenham Hotspur badala yake.

Anderlecht ilimtaka Eriksen, lakini haikuwezekana.

Ofisa huyo, Jesper Fredberg alimweleza Voetbal Nieuws: „Tulimleta Leander Dendoncker, katika nafasi ambayo ushindani wa kweli ulihitajika. Ndio maana hatukuhitaji mchezaji mwingine mwenye uzoefu katika safu ya kiungo, ingawa Eriksen alikuwa fursa kabisa, ambayo haikuwezekana. ."



Eriksen amekiri kwamba angekuwa tayari kuondoka Old Trafford kama klabu ingemwambia hakuna matarajio yoyote kwake hapo United, lakini haikuwa hivyo.

"Kama wangeniambia niondoke, ningeondoka," alisema akiiambia Manchester Evening News.

"Bado mwaka mmoja katika mkataba wangu kwa hiyo mwelekeo wangu utakuwa mwaka huu, kwenda nje na kuona nini kitatokea baadaye."

## HABARI MICHEZO

### Gamondi: Tumejiandaa kuingia makundi...

INATOKA UKURASA 24

Bacca.

Kwa upande wake, Kocha wa CBE, Leulelsegd Betsalot, alisema mchezo utakuwa mgumu kwa kuwa wanacheza na timu kubwa na yenye uzoefu wa kutosha lakini watajaribu kucheza kwa utulivu na akili kubwa.

"Dakika 90 ndizo zitakazoamua, Yanga ni timu kubwa na kwetu tunaona tuna mlima mkubwa wa kuupanda kuweza kuwatoa, lakini kwenye mpira lolote linawezekana, tutapambana kwa akili kubwa kujaribu kuwarudisha nyuma na ikiwezekana kupata ushindi," alisema Betsalot.

Endapo Yanga watafanikiwa kuwatupa nje CBE, watakuwa wamefuzu hatua ya makundi ya michuano hiyo kwa mara ya pili mfululizo baada ya mwaka jana kufika mpaka hatua ya robo fainali na kutolewa kwa mikwaju ya penalti ya Mamelod Soundowns.

### Mpanzu awasili nchini kumalizana na Simba

INATOKA UKURASA 24

upande wa pembeni, kwa hiyo mazungumzo yakaanza tena, lengo ni kumsajili ili atusaidie tukishaingia hatua ya makundi," alisema mtoa taarifa huyo.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, akikiri kuwa Mpanzu yupo nchini, lakini hakuwa tayari kusema kama ameletwa na timu hiyo.

"Sipapata mrejesho kutoka kwa mabosi wangu kam amekuja Simba au kwenye michakato yake, ila wote tunatambua dirisha la usajili limefungwa, litafunguliwa mwezi Desemba, ila ni jambo zuri kumpata mchezaji aina ya Mpanzu ili kuboresha maeneo yetu ya pembeni kulia na kushoto, waliopo waongeze juhudi zao, lakini kama kuongeza mtu mwingine kwa ajili ya kulifanya eneo hilo liwe hatari zaidi.

Ukiangalia kwenye soka la kisasa mabao mengi yanapatikana kutoka pembeni, ukiwa na watu makatili eneo la mawinga, unakuwa na matégemeo ya kupata mabao muda wowote ule," alisema Ahmed.

Taarifa zinasema kuwa bado wachezaji kama Joshue Mutale, Edwin Balua, Kibu Denis, bado hawajamshawishi kocha Fadlu Davids, akiwataka waongeze juhudi, lakini pia akiwaambia mabosi kuwa kama wanaweza kuongeza winga ambaye ana uwezo wa kupachika mabao wafanye hivyo.

# KOCHA: HII NDIYO AZAM NINAYOITAKA

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Azam FC Rachid Taoussi, ameonesha kuridhishwa na kiwango cha wachezaji wake walichokionesha juzi jioni kwenye Uwanja wa KMC Complex, Mwenge, Dar es Salaam, ilipoisasambua KMC mabao 4-0, akisema hicho ndicho kiwango alichokuwa akikihitaji.

Raia huyo wa Morocco, mara baada ya mchezo huo, alisema katika mchezo dhidi ya Pamba Jiji ambao uliisha kwa suluhu, alibainisha timu yake kucheza vyema lakini wanashindwa kufunga mabao, lakini juzi alicheza vizuri na kupachika mabao, kitu kinachoonesha kuwa mafunzo yanawaingia vizuri wachezaji wake.

"Ndicho tulichokuwa tunahitaji, nilisema wakati mwingine unaweza ukacheza vyema lakini usipate mabao kama tulivyofanya katika mchezo dhidi ya Pamba, lakini unaweza ukacheza vibaya ukapata mabao, na unacheza vizuri ukapata mabao vile vile, leo tumecheza vizuri na kupata mabao mengi, hivi ndivyo ninavyohitaji na nahitaji muendelezo katika hili," alisema kocha huyo.

Yalikuwa ni mabao ya Idd Suleiman 'Nado', akiwa ndiye mchezaji wa kwanza wa Azam kupachika bao msimu huu, akifunga dakika ya 19, Lusajo Mwaikenda, dakika ya 55, Nassor Saadun dakika ya 60 na Fredy Tangalo wa KMC alijifunga katika harakati za kuokoa.

Kwa upande wa kocha wa KMC, Abdihamid Moallin alisema wamefungwa mabao yote hayo kutokana na kufanya makosa mengi upande wa ulinzi.

"Tumefanya makosa mengi ya kiulinzi, lakini hatuwezi kuendelea kulia, badala yake tukakwenda kwenye uwanja wa mazoezi kuangalia nini tutafanya kwenye mchezo wetu unaofuata dhidi ya JKT Tanzania," alisema kocha huyo raia wa Somalia.

Kwa matokeo haya, Azam inapanda kuyoka nafasi ya 10 hadi ya sita, ikiwa na pointi tano, ukiwa ni ushindi wao wa kwanza baada ya kusuluhu mbili, huku KMC, ikiwa kwenye nafasi ya nane na pointi zake nne.



Wasanii wa kikundi cha ngoma za utamaduni Vipaji Group, kikitoa burudani wakati wa hafla ya kukabidhi tuzo za wanasayansi vijana chipukizi yaliyoandaliwa na Taasisi ya Wanasayansi Chipukizi Tanzania (YST), iliyofanyika jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mgoyi achaguliwa kuiongoza Kigoma

**Na Mwandishi Wetu,** KIGOMA

AHMED Mgoyi amechaguliwa tena kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mpira wa Miguu Mkoa wa Kigoma (KFA), katika uhaguzi mkuu uliofanyika kwenye ukumbi wa hoteli ya Lake Tanganyika jana.

Akitangaza matokeo ya uchaguzi, Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi ya KFA, Wakili Sadiki Aliki, alisema Mgoyi ameibuka mshjndi baada ya kupata kura zote za ndio.

Aliki alimtangaza Mbuya Kilima amekuwa Makamu Mwenyekiti baada ya kupitishwa na wajumbe wa Mkutano Mkui wa KFA huku Issa Bukuku akichaguliwa kuwa Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa Shirikisho cha Soka Tanzania (TFF).

Aliwatangaza waliochaguliwa kuwa wajumbe wa Kamati ya Utendaji ni pamoja na Issaya Manega na Denissa Buberwa.

Wakati huo huo Mgeni rasmi katika mkutano huo, Katibu Mkuu wa TFF, Wilfred Kidao, aliwapongeza KFA kwa kufanya mashindano mbalimbali na kuahidi shirikisho litaendelea kuwaunga mkono katika shughuli zote za maendeleo ya mpira wa miguu.

Kidao kwa upekee alitangaza kuipatia wilaya ya Kakonko mipira 50 kutokana na juhudi zao za kusimamia na kuendesha mashindano mbalimbali ambayo yameongeza hamasa mkoani humo.

Alisema pia TFF imepanga kuwekeza katika miundomimbu mkoani humo na itaanza na kujenga uwanja bora kwa ajili ya mashindano ya soka la ufukweni.

Michezo
Jumamosi Septemba 21, 2024
Nipashe



## Sterling aweka rekodi yake Uefa

UKURASA 21



Wachezaji wa Yanga wakijifua kabla ya mchezo wa leo wa Ligi ya mabingwa Afrika dhidi ya CBE kwenye uwanja wa Amaan, Zanzibar. **PICHA: YANGA**

## Mpanzu awasili nchini kumalizana na Simba

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI timu yao ikitarajia kucheza mchezo wa marudiano wa Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Al Ahli Tripoli kesho, klabu ya Simba imemshusha winga, Elie Mpanzu nchini kwa ajili ya kumalizana naye kabla ya kumtangaza kipindi cha dirisha dogo la usajili.

Habari kutoka ndani ya klabu hiyo zinasema kuwa Mpanzu aliwasili nchini juzi na tayari baadhi ya makubaliano yamefikiwa.

Imeelezwa kuwa Simba imekubali kutoa kiasi cha Dola za Marekani 200,000 ambazo ni sawa na kiasi cha Sh. Milioni 544 na atalipwa mshahara wa Sh. Milioni 27 kwa mwezi.

Awali mchezaji huyo ambaye anaichezea AS Vita ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, ilikuwa asajiliwe kipindi cha dirisha kubwa la usajili, lakini dili lilishikwa kufanikiwa, alipotimkia Klabu ya Genk ya Ubelgiji kwa majaribio, lakini mwisho wa siku alifeli.

Mtoa taarifa ndani ya klabu hiyo amesema baada ya kurejea nchini mwao, Mpanzu aliwasiliana na viongozi wa Simba ambao walionekana kutomhitaji tena, lakini kutokana na wanavyoiona timu yao, wanadhani wanahitaji winga wa aina yake.

"Mpanzu alikuwa akiihitaji sana Simba na alikuwa akipiga simu kwa viongozi kuwa sasa yupo tayari, lakini walimtolea nje, baadaye ikaonekana bado kikosi kina mapungufu hasa

INAENDELEA UK. 23

# Gamondi: Tumejiandaa vizuri kuingia makundi kwa kishindo

Kocha huyo amesema anatarajia ushindi mzuri baada ya kufanyia kazi upungufu ingawa.....

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

KOCHA wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema wamejipanga kuhakikisha wanatinga hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa kishindo kwenye mchezo wa leo wa marudiano raundi ya kwanza dhidi ya CBE ya Ethiopia.

**Kwenye mchezo wa leo, Yanga inahitaji sare au ushindi wa aina yoyote kuweza kusonga mbele kufuatia ushindi wa bao 1-0 walioupata ugenini kwenye mchezo wa kwanza.**

Akizungumza mjini hapa jana, Gamondi, alisema wamejiandaa vizuri na wapo tayari kwa ajili ya mchezo huo ingawa ameutabiri utakuwa mchezo mgumu na wenye upinzani.

Alisema anataka kuona kile alichokifanyia kazi mazoezini kinamletea matokeo chanya kwenye mchezo wake na amewataka wachezaji wake kuhakikisha wanatumia vizuri kila nafasi wanayoipata kwenye mchezo huo.

"Nimekuwa nikifanyia kazi tatizo la kukosa magoli, kwa siku za karibuni tunatengeneza nafasi nyingi lakini hatuzitumii na kujikuta kama tunashinda tunashinda kwa magoli machache, naamini kwenye mchezo wa kesho hali haitakuwa hivyo, tunataka kuona tunatinga hatua ya makundi kwa kishindo," alisema Gamondi.

Pamoja na hayo, Gamondi amesema hataki wachezaji wawe na presha kwa kuwa tayari watanguliza mguu mmoja na wanachotakiwa ni kuwa na utulivu na kucheza soka lao la kila siku akiwasisitiza zaidi kutumia vizuri nafasi.

"Wapinzani wetu hawana cha kupoteza, wapo nyuma kwa bao moja hivyo watakuja kwa kasi na kutaka kutushambulia kuweza kusawazisha bao tulilowafunga, nimewataka wachezaji wangu kuwa makini nao na kucheza kwa tahadhari licha ya kuwa tupo nyumbani," alisema Gamondi.

Wakizungumza juu ya mchezo huo, nyota wa Yanga, Dikson Job na Ibrahim Baka, wamesema wanajiandaa vizuri na mchezo huo na wapo tayari kuhakikisha wanaipeleka Yanga hatua ya makundi ya michuano hiyo kwa mara ya pili ndani ya kipindi cha miaka miwili.

"Yapo makosa madogo madogo ambayo yalionekana kwenye mchezo uliopita, benchi letu la ufundi limefanyia kazi na tupo tayari sasa kwa mchezo huu," alisema Job.

"Tunaomba mashabiki wetu wajitokeze kwa wingi kutupa sapoti, tunaamini hatutawaangusha, mashabiki wamekuwa wakitusapoti sana na hii ni nafasi nyingine ya kuwashukuru kwa kuhakikisha tunapata ushindi mzuri," alisema

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >